





UKURASA 4

**Shaka:** Maalim Seif kielelezo uzalendo nchini




UKURASA 24


# Nipashe

Ijumaa Julai 15, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581007

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Hoja 10 za CHADEMA kushuka bei mafuta



1. Ruzuku 500/- lita ya mafuta
2. Serikali kubana matumizi
3. Kuhami uhimilivu shilingi
4. Matumizi gesi kwenye magari
5. Ruzuku waagizaji wa mafuta
6. Kasi kuvutia wawekezaji
7. Mikutano kidigitali
8. Uwekezaji miundombinu gesi asilia
9. Umeme kwa wingi viwandani
10. Uzalishaji bidhaa za ndani

UKURASA 2

## Samia amkumbuka Mkapa kushirikisha sekta binafsi

UKURASA 2



Hayati Benjamin Mkapa

## Malori ya mizigo kuzuiwa kuingia D'Salaam

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA SAFARINI MISRI NA M-BET UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6




Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na viongozi mbalimbali pamoja na wageni waalikwa kwenye maadhimisho ya pili ya Kumbukizi ya Rais wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Hoja 10 za CHADEMA kudhibiti bei ya mafuta

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimependekeza mambo kumi kwa serikali ili kupunguza upandaji wa bei ya petroli na dizeli. Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, John Heche, alitoa mapendekezo hayo kwa niaba ya chama jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Heche alisema serikali inapaswa kupunguza gharama za matumizi yake na fedha hizo zielekezwe kwenye kutoa nafuu ya bei ya mafuta.

"Serikali inaweza hata kujipunguzia kodi maana zinakwenda serikalini tukaangalia kwa miezi sita. Vita vya Ukraine haviwezi kuendelea milele. Inawezekana kuondoa kodi kadhaa ili wananchi wapate unafuu.

"Mahitaji yetu kwa sasa ni takriban mapipa 60,000 kwa siku moja, hivyo kama serikali itaamua kutoa ruzuku ya Sh. 500 kwa lita ya petroli na dizeli sawa na asilimia 50 ya tozo za serikali, kutakuwa na unafuu mkubwa sana," alisema.

Heche alisema ili kufanikisha hilo, serikali itapaswa kutenga Sh. bilioni 4.8 kwa siku na kwa miezi sita hadi Desemba, mwaka huu, zitakuwa Sh. trilioni 1.8 sawa na asilimia nne ya bajeti ya serikali.

Kiongozi huyo aliyataja mapendekezo mengine ni mkakati wa muda mfupi na kati ili kuhami uhimilivu wa sarafu ya nchi, serikali kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi sawia na kuimarisha uwekezaji wa miundombinu ya matumizi ya gesi asilia kwenye magari na mitambo mingine.

Kadhalika alisema serikali inatakiwa kupunguza matumizi ya fedha za kigeni hususani kwa kubadili njia ya kushiriki mikutano nje kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Aliongeza mkakati wa muda mrefu unatakiwa kuzingatia uchumi wa uzalishaji bidhaa na huduma kwa ajili ya kuuza nje ya nchi na kuzalisha mazao mengi ya kilimo.

Pia alisema serikali inapaswa kuongeza ruzuku kwa waagizaji wa mafuta ili kupunguza gharama ya uagizaji na kuhakikisha kuna umeme wa uhakika maeneo ya uzalishaji. Alishauri serikali ichukue hatua za haraka kupunguza utegemezi wa mafuta kutoa nje kwa kuanza kutumia gesi asilia katika maeneo yote yanayoweza kutumia kwa sasa kupitia mabomba ya gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam.

**CHANZO BEI JUU**

Awali, katika uchambuzi wa bei za mafuta alisema chama kimebaini kushuka kwa thamani ya shilingi ni chanzo kikuu cha kuongezeka bei ya mafuta nchini.

"Kwa mfano kutokana na kuvurugika kwa mfumo wa uchumi toka mwaka 2015 mpaka sasa, Watanzania wanalalamika kulipa Sh. 600 zaidi kwenye lita moja ya mafuta Dar es Salaam.

"Kiwango cha sasa kwa lita moja ambacho ni Sh. 3,497 kinapaswa kupungua kwa Sh. 600, hivyo kuuzwa kwa Sh. 2,894 kabla ya ruzuku na Sh. 2,620 baada ya ruzuku," alisema.

Pia alisema uchambuzi wao umebaini kuwapo kwa visababishi vya wazi na vilivyofichika nyuma ya kupanda kwa bei za mafuta tangu Februari, mwaka huu, na kwamba sababu si vita vya Russia na Ukraine bali maandalizi mabaya namna ya kukabiliana na madhara ya UVIKO-19 na sera za kikodi.

# Samia amkumbuka Mkapa kushirikisha sekta binafsi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kumbukizi ya Hayati Benjamin Mkapa imemkumbusha wajibu na umuhimu wa ushupavu wa uongozi katika kuyafikisha mabadiliko ya maendeleo kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Aliyasema hayo jana katika kongamano la kumbukizi ya Mwasisi wa Taasisi ya Mkapa (Mkapa Foundation) ambaye alikuwa Rais wa Tanzania awamu ya tatu, lililofanyika mjini hapo.

Alisema Hayati Mkapa alikuwa muumini thabiti wa ubia kati ya sekta binafsi na serikali katika kutatua changamoto zinazomkabili.

Rais Samia alimzungumzia kiongozi huyo kuwa alikuwa na maono ya mbali kwa sababu nchi ilikuwa na imani ya kijamaa isiyoamini kushirikiana na sekta binafsi, lakini alikuwa na uthubutu na ushawishi wa kufanya kazi na sekta binafsi ingawa watu hawakumwelewa azma yake hiyo.

Alimkumbuka kwa kumnukuu maneno aliyoyasema katika hotuba yake aliyoitoa katika Halmashauri Kuu ya CCM Dodoma, Agosti 5, 2014 wakati wa uhai wake alizungumzia ushupavu wa uongozi unaohitajika katika karne ya 21.

"Katika hotuba ile pamoja na mambo mengine mengi Mzee Mkapa alituasa kuwa uongozi shupavu hauogopi kubadili mkakati iwapo ni lazima kufanya hivyo... akaendelea kusisitiza kuwa tukishaamua sera tunahitaji ujasiri wa kutenda na sio kwa maneno, ukiwapo ubishi uwe wa kasi na ubora wa utendaji na sio tena ubishi wa sera tuliokwisha uamua," alisisitiza Rais Samia.

Akizungumzia maono ya Hayati Mkapa, Rais Samia alisema, bado watu wanaendelea kubishana na sera badala ya kasi na ubora wa utendaji katika kuikumbatia sekta binafsi bado baadhi ya viongozi hawajaamini kuwa sekta binafsi ni mshirika muhimu katika kuleta maendeleo.

Rais Samia alisisitiza kurejea kuyasema maneno hayo ya Mkapa kuonesha maono yake katika ushupavu na ustahamilivu katika uongozi kwa sababu hakuogopa kusema ukweli wa kwamba dunia ya sasa ni ya uchumi na soko na kwamba ubia na sekta binafsi ni jambo lisiloepukika.

"Sasa serikali tumelitambua hilo na kuliainisha katika mikakati yetu ya maendeleo ya kitaifa ndani ya nchi yetu ikiwamo pia katika mpango wa mkakati wa tano wa afya, tutashirikiana na sekta binafsi ikiwamo asasi za kiraia katika kufikia malengo ya maendeleo na kuwafikishia wananchi huduma bora za afya popote walipo na kwa gharama nafuu," alisema.

Aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuanza vyema kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma ya afya kwa wananchi.

Alisema kuwa ili kwenda kwa kasi na kufikia lengo la afya kwa wote lazima kubadilisha mitazamo kwa kuishirikisha sekta binafsi na sio kuiachia serikali pekee.

**SEKTA BINAFSI IAMINIWE**

Rais Samia alionyesha kusikitishwa na kinachoendelea nchini, kuwa sekta binafsi inaifuata serikali kutaka ushirikiano, lakini wanazungushwa mpaka wanakata tamaa. Alisema tayari ameshapokea maombi kuwa sekta binafsi inataka kuweka mitambo ya vipimo vya afya katika maeneo kadhaa ya Tanzania, lakini hakuna anayewasikiliza wala kupewa ushirikiano.

**VIATU NI VIKUBWA**

Naye Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema wakati alipofuatwa kuombwa kuwa msarifu (kiongozi) wa Mkapa Foundation alipatwa na kigugumizi kilichotokana na shaka kuwa viatu anavyovivaa ni vikubwa ikizingatiwa kuwa msarifu wa kwanza ni mwenyewe hayati Mkapa, lakini hakuwa na uthubutu wa kukataa.

Alisema alipata nguvu zaidi ya kukubali kuongoza taasisi hiyo kwa kukumbuka kwamba matunda ya kazi zinazofanywa na taasisi hiyo zinalenga kuimarisha ustawi wa Tanzania na kazi njema lazima ziendelezwe.

Alisema kazi njema iliyoanzwa na taasisi hiyo ni njia bora na sahihi ya kumuenzi na kumkumbuka muasisi wa taasisi hiyo na kwa kutambua dhima na jukumu alilopewa amejizatiti kuongoza taasisi hiyo na kuhakikisha dira na dhamira ya kuanzishwa kwake inafikiwa.

Serikali yake, alisema imeweka kipaumbele cha kuimarisha sekta binafsi pamoja na asasi za kiraia katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Aliipongeza taasisi hiyo kwa ushirikiano unaoendelea kutoa kwa serikali zote mbili katika kuimarisha huduma mbalimbali hasa sekta ya afya.

Alisema kuwa ushirikiano mzuri uliokuwapo baina ya serikali na sekta binafsi umesaidia kupambana na maradhi ya UVIKO-19 na taasisi mbalimbali zinaendelea kushirikiana na serikali katika upatikanaji wa vipimo, vifaa tiba, utoaji wa chanjo, elimu ya kinga pamoja na ukusanyaji wa takwimu.

Pia mafanikio hayo yamezidisha imani ya wananchi umuhimu wa serikali kushirikiana na sekta binafsi sio kwa uwekezaji pekee bali pia katika utoaji wa huduma za jamii.

"Wakati tunamkumbuka marehemu mzee Mkapa nachukua nafasi hii kugusia kidogo kuhusu falsafa na usia aliotuachia kuhusu ujasiri na changamoto za kifalsafa...katika kitabu chake alichokiandika cha My Life akizungumzia ugumu aliokutana nao katika kufanya mageuzi ya ubinafsishaji hayati Mkapa aliandika yafuatayo naomba kumnukuu kuwa kiongozi kunahitaji kuwa tayari kubadilika, kulingana na mawazo mapya na kuwa na ujasiri wa kutekeleza yale yaliosahihi mwisho wa kunukuu," alisisitiza.

Aidha, ushupavu huo wa uongozi unadhihirisha pia maneno ya muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume aliyosema: 'Ni heri kugombana na mtu katika jambo litakalokuja kupatana baadaye'.

Alisema kwa kawaida mageuzi kama yalivyo mapinduzi huja na mafanikio na changamoto zake ni hulka ya binadamu kupenda kushikilia jambo alilolizoea hata kama halina faida huku akirejea maneno ya wahenga 'mazoea yana tabu'.

Kwa upande wake Rais mstaafu wa Msumbiji, Joacquim Chissano, alisema hayati Mkapa alikuwa ni rafiki yake wa karibu wakati wa uhai wake na alishirikiana naye kuunganisha watu wa Msumbiji na Tanzania.

Alisema Mkapa alikuwa na ushirikiano, umoja na mpaka wanatangaza uhuru mwaka 1966 na kushirikiana katika ukombozi wa nchi za Afrika, walishirikiana katika biashara, uchumi huria, vyama vingi vya siasa na kupata maendeleo katika nchi zao.

# Tanzania yapokea dozi milioni tatu chanjo ya corona

**Na Romana Mallya**

SHEHENA nyingine ya chanjo aina ya Sinopharm dozi milioni tatu zimeingia nchini ambazo zitawakinga Watanzania 1,500,000 dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Chanjo hizo zimetolewa kwa hisani ya mke wa Rais wa China, Prof. Peng Liyuan.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam baada ya kupokea chanjo hizo, Mkurugenzi wa Kinga, Wizara ya Afya, Dk. Beatrice Mutayoba, alisema mpaka sasa zilizotolewa kutoka China zimefikia dozi 6,000,000.

Alisema chanjo hizo zimethibitishwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) na kuwataka wananchi wachanje kwa sababu ili kufikia kinga jamii ni lazima asilimia 70 ya walengwa ambao ni watu 21,518,649 wawe wamechanja.

Dk. Mutayoba alisema hadi kufikia Julai 12, mwaka huu, Watanzania 10,511,804 sawa na asilimia 32.91 walikuwa wamekamilisha dozi ya UVIKO-19 na zilizopokelewa ni 21,226,520.

Mkurugenzi wa masuala ya wanawake Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Watoto na Makundi Maalum, Grace Mwangwa, alisema ni wajibu wao kuona wanawake wanapewa umuhimu katika suala hilo kwa sababu ndiyo wanaothirika kwa kiasi kikubwa pamoja na makundi maalum.

Mwakilishi wa Balozi wa China nchini Tanzania, Chu Kun, alisema mke wa Rais wa China Prof. Peng, amependekeza kutoa chanjo kwa wanawake, watoto na vijana katika nchi 53 za Afrika na sehemu ya chanjo hiyo itatolewa kwa kundi hilo nchini Tanzania.

Alisema Rais wa China Xi Jinping, aliomba kusaidia nchi zinazoendelea na serikali yake imefanya hivyo.

Alisema hadi sasa China imetoa zaidi ya dozi bilioni 2.2 za chanjo kwa zaidi ya nchi 120 na mashirika ya kimataifa na itatoa dozi bilioni 1 kwa Afrika, ikiwa ni pamoja na asilimia 60 kama mchango wake.

# Vita Ukraine vyatoa funzo uzalishaji bidhaa za ndani

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imesema vita vya Ukraine na Russia vimeyaaibisha mataifa mengi ya Afrika, ikiwamo Tanzania, kuonyesha yalivyo tegemezi kwa bidhaa mbalimbali zikiwamo ngano na mbolea.

Imesema nchi ina rasilimali za kutosha ikiwamo ardhi yenye rutuba lakini bado inaishi kwa kutegemea kuagiza bidhaa nje ya nchi. Kwa utegemezi huo, inamaanisha kuwa inaishi kwenye zama za utumwa na haijapata uhuru wa kiuchumi.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mazungumzo yake na wanachama wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI).

Alisema nchi za Afrika zimejaliwa kuwa na ardhi kubwa yenye rutuba na rasilimali nyingi ambazo zingewezesha kuzalisha bidhaa kwa wingi na kuuza nje, lakini inashangaza kuona bado zikitegemea bidhaa nyingi kutoka nje ya nchi. Baada ya vita hivyo kuanza, alisema mataifa mengi ya Afrika yalianza kulalamikia uhaba wa ngano na mbolea wakati zimebarikiwa kuwa na ardhi ya kutosha yenye rutuba na rasilimali nyingi ambazo wangezitumia kuzalisha bidhaa nyingi.

"Kwa vita hii, Mungu ametupa funzo tujifunze kujitegemea ni aibu kubwa kuona watu wa Afrika tunaokadiriwa kufika bilioni moja kulalamikia uhaba wa ngano na mbolea. Hivi vita vimetuvua nguo kwani vimeonyesha kumbe wote tunategemea kuagiza ngano na mbolea Ukraine wakati tuna kila kitu cha kutuwezesha kuzalisha wenyewe," alisema.

Alisema viwanda vya kuzalisha mbolea nchini vinatosheleza asilimia tatu tu ya mbolea inayohitajika, hivyo akatoa wito kwa wenye viwanda kuwekeza zaidi kwenye uzalishaji ili kuondokana na utegemezi wa bidhaa hiyo kutoka nje. Waziri alisema serikali imejitahidi kwa kiwango kikubwa kuweka mazingira mazuri ya biashara kuwawezesha wawekezaji kuzalisha kwa wingi na kwenye mazingira ya ushindani, hivyo wanapaswa kuchangamkia fursa hiyo.

"Huu umaskini tulio nao ni wa kujitakia kwa sababu tuna kila kitu na serikali imedhamiria kwa dhati kuiinua sekta binafsi mkue kwa kasi. Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) aliponiteua, aliniuliza kwa nini sekta binafsi haikui ipasavyo. Akaniambia nakupa miezi sita uje unijibu hili swali, kwa hiyo nawahakikishia fanyeni kazi sisi tunaendelea kuwawekea mazingira mazuri," alisema.

Pia alisema viwanda hivyo vinapaswa kuwekeza zaidi kwenye kuongeza thamani ya malighafi zinazozalishwa nchini na kuuza bidhaa badala ya kusafirisha malighafi nje ya nchi. Alisema kufanya hivyo ni sawa na kusafirisha ajira za Watanzania.

Alisema serikali imejitahidi kuondoa vikwazo vyote vya kikodi ili kufungua masoko mbalimbali ya Mashariki, Kusini mwa Afrika na Afrika kwa ujumla, hivyo kilichobaki ni kwa wafanyabiashara wenyewe kufanya kazi.

Mwenyekiti wa CTI, Paul Makanza, aliiomba serikali kulinda viwanda vya ndani kwa kuhakikisha inatoza kodi stahiki kwa bidhaa zinazotoka nje ili kufanya bidhaa zinazozalishwa nchini na zinazoagizwa nje kuwa na ushindani halali.

Alisema CTI inafurahi kuona utayari wa serikali kufanya kazi kwa karibu na sekta binafsi huku akiipongeza kwa kuwekeza zaidi kwenye miundombinu ya barabara na reli ambayo ni muhimu kwa ajili ya kusafirisha bidhaa kutoka sehemu moja hadi nyingine hususan zinakozalishwa hadi kwenye masoko.

# Malori ya mizigo kuzuiwa kuingia Dar es Salaam

**Na Martha Magawa**

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) umesema uko mbioni kuzuia malori makubwa kuingia mjini Dar es Salaam, badala yake yataanzia Kibaha mkoani Pwani ambako kunajengwa bandari kavu.

Ili kutekeleza mpango huo, wakala huo umesema mizigo itakuwa inatolewa na kuingizwa mkoani Dar es Salaam kwa kutumia treni.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam, Harun Senkuku, akizungumza na Nipashe juzi ofisini kwake mkoani hapo, alisema suala la kuondoa magari makubwa katikati ya mji litakamilika kabla ya mwaka 2025.

Senkuku alisema lengo la TANROADS ni kuhakikisha inapunguza magari ya mizigo katikati ya mji kama siyo kuyaondoa kabisa kwa kuwa tayari ujenzi wa barabara za pembezoni unaendelea katika maeneo yote nchini.

"Barabara zetu nchini ni za matumizi ya wote, vyombo vya moto na binadamu. Mbali na kusababisha foleni, malori ya mizigo ni hatari na tumeshuhudia mara nyingi yakisababisha madhara ikiwamo vifo," alisema Senkuku.

Kwa kurejea miezi miwili iliyopita, lori la aina hiyo lilisababisha vifo vya aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Dar es Salaam, Prof. Honest Ngowi na dereva wake mkoani Pwani.

Senkuku pia alibainisha kuwa katika kutekeleza hilo, vituo vya mabasi ya mikoani viliondolewa katikati ya miji na kujengwa pembezoni mwa miji, lengo likiwa kubaki na magari madogo katikati ya miji.

"Mizigo mikubwa itakuwa haitembei tena kwenye barabara za kawaida ambazo ziliharibiwa zaidi na kuzidiwa matumizi. Ikifika Kibaha, itatumika reli ya kisasa (SGR) kuingia na kutoka jijini Dar es Salaam," alifafanua.

Katika mazungumzo hayo na Nipashe, Senkuku pia alitoa ufafanuzi kuhusu mchakato wa ujenzi wa barabara za kulipia (express ways) kuanzia Kibaha mpaka Morogoro ambazo dereva, kwamba zitasaidia kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara hiyo.

Alisema kuwa barabara hizo ambazo dereva atapaswa kulipia gharama ya ziada na kutembea mwendo anaotaka yeye, ziko katika hatua za mwishoni na muda wowote kuanzia sasa zitaanza kujengwa.

"Tunapoelekea kujenga barabara za viwango vya kimataifa, tutaongeza 'express ways' ambapo madereva wanaohitaji mwendo wa ziada watapita huko na kutakuwa na gharama ili kupita katika barabara hizo.

"Tumejipanga kudhibiti pia madereva wasio waadilifu ambao wamekuwa pia wakipita wasikotakiwa kupita, mfano barabara za mabasi yaendayo haraka mkoani hapa," alisisitiza.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **TAUSI AUCTION MART & COMPANY LIMITED, JOSINA AUCTION MART & COMPANY LIMITED, MASE INTERANATIONAL LIMITED, BILO STAR DEBT COLLECTOR LIMITED na MANGWEMBE 2011 CO. LTD** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD.** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo

| | NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|---|
| | TAUSI AUCTION MART & COMPANY LIMITED | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | STEPHANO E SABUNI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | FOREST - MOROGORO |
| 2 | ISSA K YUSUPH | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIYEGEYA - MOROGORO |
| 3 | GRANT R MUSHI | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MASEYU - MOROGORO |
| 4 | ZUWENA M MFIKIWA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MGULU-MOROGORO |
| 5 | SAFINA SELEMAN KONGERA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | CHAMWINO-MOROGORO |
| | JOSINA AUCTION MART & COMPANY LIMITED | | |
| 6 | KIBIA J WILSON | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIMUSI - TARIME |
| 7 | SWAIBA ALEX MWITA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MSETI - TARIME |
| 8 | BENJAMIN JOHN BWITANI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MSETI B- TARIME |
| 9 | SHADRACK M CHACHA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | BIAMBWI - TARIME |
| 10 | SAMWEL FRANCIS NYAMASATI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | REBU - TARIME |
| | MASE INTERNATIONAL LIMITED | | |
| 11 | SAMWEL W CHACHA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KEBIKIR I-TARIME |
| 12 | MARTIN M MWENDESHA | KIWANJA CHENYE OFFER NO.311, KITALU A MD | TINDE - MIZANI-KAHAMA |
| 13 | STEVEN DAUDI GARAIRE | BOMA LENYE MKATABA WA MAUZIANO | NKENDE - TARIME |
| | BILO STAR DEBT COLLTOR COMPANY LIMITED | | |
| 14 | CHAPEWA PATRICK MWISUA | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI NO. 468,KITALU H MALI YA MDHAMINI YENYE MAJINA ALICE MICHAEL BENEDICT | GOBA - DAR ES SALAAM |
| 15 | FROLA RAFAEL MWANDUPE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | SALASALA - DAR ES SALAAM |
| | MANGWEMBE 2011. C0.LTD | | |
| 16 | FRANK BONIPHACE MWACHA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBEZI-MSUMI - UBUNGO-DAR ES SALAAM |
| 17 | PETER RODRICK NGOWO | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | BONYOKWA - DAR ES SALAAM |
| 18 | ELIA M KIVUYO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | UBUNGO-MSEWE - DAR ES SALAAM |
| 19 | FATUMA M MJEMA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | ENGOSENGEU - ARUSHA |
| 20 | ROBERT L MKENDYA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | NGORBOB - ARUSHA |
| 21 | LOISHIYE E MOLLEL | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | EMATASIA - ARUSHA |
| 22 | ELIZABETH J KITIKA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAWAUZIANO | MLIMANI - ARUSHA |
| 23 | MOHAMED MICHAEL KITUNGULU | NYUMBA YENYE HATI MILIKI YA KIWANJA NO.289, KITALU F | JOGOO - IFAKARA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atakayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipwa kulingana na makubaliano yatakayofikiwa kati ya benki na mnunuzi.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mkurugenzi Mtendaji Tausi Auction Mart & Company Limited S.L.P Dar es Salaam Namba za simu: 0692926969 NA | Mkurugenzi Mtendaji. Josina Auction Mart & Company Limited S.L.P MWANZA Namba za simu; 0713203040/ 0789203040 NA | Mkurugenzi Mtendaji, Bilo Star Debt Collector LimitedS.L. P Dar es Salaam Namba za simu: 0716943424 NA | Mkurugenzi Mtendaji, Mangwembe 2011. CO..Ltd S.LP Arusha Namba za simu; 0752632033 NA | Finca Microfinance Bank Ltd P.O. Box 78783 Namba za simu: 0768790399, 0754774949 |

216945501



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka (wa tatu kulia), akishiriki dua iliyosomwa kwenye kaburi la aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, akiwa katika ziara ya kichama Kisiwani Pemba, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shaka asema Maalim Seif kielelezo uzalendo nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, amesema aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Shariff Hamad, ni mfano wa kuigwa katika kufanya siasa za uvumilivu na maslahi kwa taifa.

Shaka aliyasema hayo jana Mtambwe, kisiwani Pemba, alikokwenda kuzuru kaburi la mwanasiasa huyo mkongwe, aliyefariki mwaka jana.

"Wakati tunamkumbuka ndugu yetu huyu aliyetangulia, Tanzania inaadhimisha miaka 30 toka kuanzishwa mfumo wa vyama vingi. Maalim Seif ana mchango mkubwa sana katika mafanikio haya," alisema na kuongeza:

"Kila mara CCM tulipoanzisha mchakato wa maridhiano, Maalim Seif alikuwa tayari kushiriki.

Aliweka mbele maslahi ya nchi, kwa hakika ni kiongozi wa mfano wa kuigwa."

Shaka alisema Maalim Seif ameliachia taifa deni kubwa ambalo ni kuendeleza amani na mshikamano. "Ndugu zangu tuna deni kubwa alilotuachia Maalim Seif ambalo ni amani na utulivu. Leo (jana) tumekuja hapa sote bila kujali itikadi zetu wala dini zetu. Hii ni kwa sababu ya kazi kubwa aliyoifanya Maalim Seif ya kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa," alisema.

Naye mdogo wa Marehemu Maalim Seif, Zubeir Hamad Sharif, alimshukuru Shaka kwa kufika kaburini hapo kumwombea marehemu kaka yake.

"Nakushukuru sana. Wewe (Shaka) ni kiongozi wa kitaifa una shughuli nyingi lakini umetenga muda kuja hapa. Mwenyezi Mungu akulinde" alisema.

Shaka ambaye yuko katika ziara ya siku mbili kisiwani Pemba, anakuwa kiongozi wa kwanza wa ngazi ya juu wa CCM kuzuru kaburi la Maalim Seif aliyefariki Februari, mwaka jana.

Awali, Shaka alizuru kaburi la aliyekuwa Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Omar Ali Juma, Chake Chake, kisiwani Pemba na kutaka aenziwe kwa mazuri aliyoyapigania.

Akizungumza kaburini hapo kabla ya kushiriki dua ya kumwombea Marehemu Dk. Omari, Shaka alisema mwaka huu Dk Omari ametimiza miaka 21 tangu kifo Julai, 2001, huku nchi ikitimiza miaka 30 ya mfumo wa vyama vingi.

"Hapa si sehemu ya kutoa hotuba lakini ujumbe wangu ni kwamba mwaka huu tunatimiza miaka 21 tangu Dk. Omar alipotutoka. Alikuwa nguzo muhimu kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

wakati wote na kwa nafasi zote alizoaminiwa alitimiza majukumu yake kwa uzalendo mkubwa," alisema Shaka.

Alisema wakati Watanzania wakimwombea kiongozi huyo, pia wamwombee Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ameendeleza ndoto na za viongozi waliotangulia akiwamo Dk. Omar.

Awali, akizungumza kabla ya dua hiyo, mwakilishi wa familia ya Dk. Omar, Zubeir Ali Juma, alishukuru na kukupongeza kwa uamuzi wa Shaka na viongozi mbalimbali kwa kuzuru kaburi hilo mara kwa mara.

Viongozi mbalimbali walishiriki dua hiyo ambapo Ofisi ya Mufti iliwakilishwa na Mratibu wa Ofisi hiyo Pemba, Shekhe Said Ahmad Mohamed na madhehebu ya Kikristo, yaliwakilishwa na Mchungaji Benjamin Kisanga wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Pemba.

# Mwigulu ataka kufumuliwa sheria kikwazo kwa mfumo mpya ununuzi

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameiagiza Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), kuboresha sheria zote zinazokinzana na mfumo huo mpya wa ununuzi ili kufikia lengo la serikali la kuepuka kupoteza fedha nyingi.

Dk. Nchemba alitoa agizo hilo jana Jijini Dar es Salaam, wakati wa hafla ya kumuaga aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Balozi Dk. Matern Lumbanga.

"Ninasisitiza kuwa isije ikatokea tukatumia kichaka cha sheria kutukwamisha katika utekelezaji wa maelekezo haya. Sheria ambazo zinatukwamisha katika juhudi za kustawisha maendeleo ya Watanzania na zinalinda wezi za Watanzania hazitufai," alisema.

Pia aliagiza kuboreshwa kwa Mfumo wa Kutangazia Tenda wa TANePS ili uweke bei za ukomo kwa bidhaa na huduma zinazotumika serikalini hatua ambayo itasaidia wanaotoza bei za juu washindwe kupata zabuni.

Alisema kati ya maeneo ambayo alielekeza yazingatiwe wakati wa kusoma Bajeti ya Serikali ya 2022/23 Bungeni, jijini Dodoma, ni kudhibiti ununuzi na matumizi ya magari ya serikali na ununuzi wa mafuta na vipuri, pamoja na matengenezo ya magari.

"Umefika wakati sasa wa kuangalia upya utaratibu wetu tunaoutumia katika ununuzi wa magari. Kwa nini nchi nyingine za jirani pamoja na mashirika ya Kimataifa kama UNDP wananunua magari kwa bei nafuu (pengine zaidi ya nusu) kuliko sisi serikalini," alisema Dk. Nchemba.

"Ni vyema serikali kuweka bei elekezi katika bidhaa na huduma inazonunua. Na tunaitegemea zaidi PPRA kutusaidia kutukwamua kutoka hapa, ndani ya kipindi cha miezi michache katika mwaka huu wa fedha, shirikianeni na taasisi nyingine," alisisitiza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Eliakim Maswi, alisema wameshaanza kazi ya kuhakikisha ununuzi wa bidhaa na huduma unazingatia bei ya soko na wapo katika hatua za mwisho za kuweka bei elekezi kwa bidhaa mbalimbali.

Alisema wamebaini kuwa, gharama kubwa za ununuzi wa magari yanayotumika zaidi serikalini, zinatokana na kuwapo kwa Wakala (dealer) mmoja nchini.

Pia alisema wanajenga upya mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS). "Kupitia kazi hii, tunatarajia mfumo huu utawezesha kuwekwa kwa bei elekezi za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumika serikalini, kupunguza muda na gharama za kuendesha michakato ya zabuni, na kuondoa urasimu katika mchakato wa ununuzi."

Naye Balozi Lumbanga, alisema mambo yanayokwamisha maboresho katika sekta hiyo ya ununuzi wa umma ni kugubikwa na vitendo vya rushwa na udanganyifu. Alisema pia usimamizi dhaifu wakati wa utekelezaji wa miradi au mikataba, taasisi nyingi kufanya manunuzi yake nje ya mfumo wa TANePS kinyume na sheria pamoja na maelekezo ya serikali na michakato ya ununuzi kutumia muda mrefu.

# ACT yawasilisha kero za wananchi mezani kwa DC

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimewasilisha mezani kwa Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, matatizo yaliyoibuliwa na wananchi yanayohusiana na sekta za miundombinu, afya na masuala ya machinga na bodaboda.

Naye Jokate amekihakikishia chama hicho kuwa matatizo hayo ambayo yaliibuliwa na wananchi kupitia ziara iliyofanywa na Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, kwenye Jimbo la Mbagala, kwa siku nane kuanzia Juni 29, mwaka huu, serikali inaendelea kuyafanyia kazi.

Katika mazungumzo hayo na Mkuu wa Wilaya yaliyofanyika jana, Shaibu aliambatana na Katibu wa Fedha na Miradi, Rachel Kimambo, Mwenyekiti wa Mkoa wa Dar es Salaam, Renatus Pamba na Mwenyekiti wa Jimbo la Mbagala, Muhdeen Nkwera.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano wa Umma, ACT-Wazalendo, Janeth Rithe, Katibu Mkuu wao Shaibu amemtembelea Mkuu wa Wilaya hiyo kwa ajili ya kubadilishana naye mawazo kuhusu matatizo hayo.

"ACT-Wazalendo tumeshakutana na Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu masuala mbalimbali ya mwelekeo wa nchi kisiasa.

"Leo (jana) nimewaleta viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kuzungumza na Mkuu wa Wilaya ya Temeke. Binafsi ninaamini kuwa tunao wajibu wa kubadilisha siasa za nchi kwenda kwenye siasa za mkazo wa masuala ya wananchi.

Alisema hilo linahitaji ushirikiano wa karibu na viongozi wa serikali katika kubadilishana mawazo na taarifa.

Akijibu hoja zilizoibuliwa, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate amemshukuru Katibu Mkuu huyo kwa kumtembelea na kuwasilisha matatizo hayo kwake.

"Kuhusu barabara ya Nzasa-Kilungule-Buza, nilifanya mazungumzo na mkandarasi. Ameshalipwa. Ni matumaini yangu kuwa itakamilishwa kwa wakati.

Pia alisema wanatarajia kupata awamu nyingine ya mradi wa DMDP ambao utaneemesha barabara nyingi zilizolalamikiwa.

# TEF yataka kasi mchakato mabadiliko sheria ya habari

**Na Mary Geofrey**

MWENYEKITI wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, amemwomba Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, kuharakisha mchakato wa mabadiliko ya sheria kandamizi katika tasnia ya habari ndani ya mwaka huu, kama alivyoahidi.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam, Balile alisema kasi ya mchakato wa mabadiliko ya sheria hizo kwa sasa umepoa hivyo kutia shaka mafanikio yake kama ilivyotarajiwa na serikali.

"Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akitoa msukumo mkubwa ili kuhakikisha wanashirikisha wadau wa habari na serikali kuhakikisha sheria zinarekebishwa. Tulikwenda vizuri hapo mwanzo, lakini baada ya Mei 3, mwaka huu (Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani), tunaona kama kasi imepungua kidogo.

"Tungependa kujua wizara ilikuwa imepanga kufanya mikutano kadhaa na kujadiliana na wataalamu wa tasnia hii, lakini sasa tunaona kama kila kitu kimesimama na tunapoendelea kuuliza, tunaambiwa bado mikutano ipo," alisema Balile.

Alisema mabadiliko ya sheria hizo bado ni muhimu kwa mazingira ya sasa huku akipendekeza kasi iongezeke ili hoja hiyo ipelekwe bungeni.

"Bado tunazihitaji sheria, bado tunahitaji hayo mabadiliko haraka kadri inavyowezekana kuliko wakati wowote ule kwa sababu, tukipitwa na lile bunge la mwezi wa tisa, ina maana tutasubiri mwaka mmoja baadaye. Bunge la mwezi wa tisa ndio la miswada," alisema.

Pamoja na kuchelewa huko, Balile alisema iwapo wizara yenye dhamana ikiamua kuongeza kasi katika mchakato huo, upo uwezekano mkubwa wa kufikia malengo ndani ya muda mwafaka.

"Tunachotafuta zaidi ni haki ya kupata habari na uhuru wa vyombo vya habari. Huu uhuru unawezesha haki nyingine kupatikana. Mfano demokrasia na vingine vyote vinavyozungumzwa, vinatokana na uhuru wa watu kutoa mawazo yao.

"Inapokuwa uhuru haujalindwa kisheria, basi unachelewesha hivi vingine kupatikana katika jamii. Huu ni mjadala na mchakato tunaopaswa kushirikishana tulio wengi kwa pamoja," alisema.

Hata hivyo, Nape akizungumza katika Mkutano wa Wadau wa Maendeleo kusaidia ukuaji wa habari juzi, alisema serikali imetoa nafasi kwa wanahabari kuwasilisha mbadala wa maoni yao na kwamba bado lengo ni kukamilika mchakato huo kwa muda mfupi.

Naye Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema serikali imeonyesha dhamira ya kutaka kupitia upya sheria na taratibu zote zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari 2016.

---

## MUHIMBILI NATIONAL HOSPITAL

# VACANCY ANNOUNCEMENT

Muhimbili National Hospital in collaboration with Emory University has received a Grant from Abbott Fund Tanzania for implementation of activities under the Emory Muhimbili Partnership for Health Administration Strengthening and Integration of Services (EMPHASIS).

To effectively implement its 5 years Corporate Strategic Plan the Hospital has planned to strengthen its Resources Mobilization base and therefore wishes to recruit 1 Resource Mobilization Officer and 1 Grant Management Officer for 1 year contract (renewable upon mutual agreement and availability of fund)

**1.0 RESOURCE MOBILIZATION OFFICER (1 POST)**

**1.1 JOB SUMMARY**

Reporting to the Head of Strategy and Business Development, the Resource Mobilization Officer shall be responsible for overall oversight and coordination of development partners engagement and proposal development. She/ He will work with all other staff to develop and submit high quality institutional and high value donor proposals that are aligned with defined MNH priorities, demonstrate impact, and other value for money. She/ He will be responsible to build the capacity of MNH to develop and manage strategic consortium partnerships with Local and International institutions, NGO, private sector organizations and individual philanthropists.

**1.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. To be a focal person in implementation of MNH Resource Mobilization Strategy;
ii. To network, update and liaise with key in-country and international development partners;
iii. To provide effective coordination for the establishment of proposal development working groups with representatives from key stakeholders within and outside MNH;
iv. To advise Hospital Management and business development teams and working groups on relevant development partners requirements/ compliance, potential funding opportunities, changes in development partners' priorities and ensuring quality grant management for all related projects;
v. To interface with Public Relations Unit for development partners mapping and communication;
vi. To act as the interface between Finance Department and program/ project teams to ensure grant compliance;
vii. To ensure fundraising staff have individual work plans and up to date development plans;
viii. To work closely with all the funding affiliates and relevant program departments to ensure high quality and timely submission of proposals and concept notes, Project Report/ Project Progress Reports to donors and funding affiliate.
ix. With support from clinicians, Head of Research, Training and Consultancy Unit and Hospital Management, to identify and facilitate opportunities for relationship building with key stakeholders;
x. To develop and manage strategic consortium partnerships with appropriate universities, NGOs and health facilities;
xi. To perform any other resource mobilization related duties.

**1.3 QUALIFICATIONS AND EXPERIENCE**

Holder of bachelor degree in social sciences majoring in one of the following fields; marketing, business administration, economics, statistics, project planning and management.

Candidate possessing Master's degree in public health shall have an added advantage. Minimum of 2 years working experience as a resource mobilization officer or marketing officer in NGO or Research institution.

**2.0 GRANTS MANAGEMENT OFFICER – (1 POST)**

**2.1 POSITION SUMMARY**

The Grants Management Officer will be a critical member of the TRCU team, reporting to the Head of Teaching, Research and Consultancy Unit. The Grants Management Officer works across all internally or externally funded programs, including collaborating with finance and IT to ensure effective and efficient grant implementation processes. The overall responsibility is to effectively manage a portfolio of grants and provide support to grant holders in order to facilitate the delivery of quality projects on time and on budget.

**2.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Monitor grants for legal, financial, and program compliance including but not limited to ensuring that grant requirements are correctly documented in the grant files and database.
ii. Review reports and monitor progress of projects to verify that grant holders are implementing grants to address agreed objectives in a timely manner and in-keeping with good practice;
iii. Work closely with colleagues to coach and support grant holders in the management of their activities, funding and partnership;
iv. Maintain regular communication with grant holders to ensure compliance to the funding organizations other Foundation professionals through Peak
v. Monitor and document the grant making workflow processes, forms, templates, reports and data to assure full compliance with internal controls and legal requirements.
vi. Generate reports and data analysis of the activities by different programs
vii. Work with finance department to ensure all payments to grant holders are executed in a timely fashion
viii. To facilitate the finance departments to generate reports required for compliance and financial statement audits by donors.
ix. Assist in developing narratives and financial report templates for grant holders.
x. Improve the way staff report progress on their grant activities by providing support and tools for reporting
xi. Participate in scheduled meetings for reporting grants progress including provision of work-related updates.

**2.3 QUALIFICATIONS AND EXPERIENCE**

i. Holder of bachelor degree in one of the following fields; statistics, Epidemiology or Public Health.
ii. Minimum of 2 years working experience as a grant management officer in NGO or Research institution

**3.0 MODE OF APPLICATION**

A signed application letter with certified copies of academic certificates and up-to-date Curriculum Vitae (CV) with three referees with reliable contacts, postal address, e-mail, and mobile numbers should be addressed to

**Executive Director,**
**Muhimbili National Hospital,**
**P.O.Box 65000,**
**Dar Es Salaam**

via the following email address:

**Email: hrt@mnh.or.tz**
**Application Deadline: 22th July, 2022**

---

Muhimbili National Hospital in collaboration with the German Society of Tropical Surgery (DTC) is seeking a highly motivated full-time Research Assistant to join the team and provide key support to the new Children Surgery Research project . This project is funded by Else Kröner Fresenius Stiftung (EKFS). This project aims at improving care of children born with surgical conditions in particular Gastroschisis in Tanzania.

**1.0 RESEARCH ASSISTANT (1 POST)**

**1.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Support ethics applications, required Data Transfer Agreements and approvals as required for running the project as well as storage of all project documents including approvals, IRBs and reports
ii. Manage data collection, data entry, report preparations and documentation of information needed for the project
iii. Assist in making sure that monitoring and evaluating process is adhered to as well as stock keeping of project supplies and equipment
iv. Establish project work plan and calendar or schedules for implementation in selected centers of Tanzania
v. Be a liaison with study sites and project leaders (Principal Investigator and Project Managers) to ensure timely and quality achievements of the project deliverables
vi. Be responsible for the organizing trainings at different sites in Tanzania
vii. Source information required to embark on the projects i.e venue, participants, catering, practical consumables, procurement requisitions, prepare travel reimbursements requests, cost transfers and monitor project financial expenditures
viii. To participate in wider Global Children Surgery Research activities such as Grand Rounds, team meetings, conferences etc.

**1.3 QUALIFICATIONS AND EXPERIENCE**

i. Holder of bachelor degree in one of the following fields: Medicine, Nursing, Pharmacy or Medical Laboratory who has completed internship and registered by reputable council.
ii. Minimum of 2 years working experience as a Research Assistant officer in NGO or Research institution

**3.0 MODE OF APPLICATION**

A signed application letter with certified copies of academic certificates and up-to-date Curriculum Vitae (CV) with three referees with reliable contacts, postal address, e-mail, and mobile numbers should be addressed to
**Executive Director,**
**Muhimbili National Hospital,**
**P.O.Box 65000,**
**Dar Es Salaam**

via the following email address:

**Email: hrt@mnh.or.tz**
**Application Deadline: 22th July, 2022**

216944001

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bei ya vyakula inaumiza hatua zichukuliwe

**BEI** ya vyakula inazidi kupanda kwa kile kinachoelezwa kuwa kupanda kwa mafuta ambayo kwa sasa lita moja ya petroli inauzwa Sh. 3,200, na dizeli ni Sh. 3,143, pamoja na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha mvua kuwa chache.

Kwa sasa unga wa ugali umepanda kutoka Sh. 1,000 kwa kilo hadi 2,000, huku dagaa wakipanda kutoka 6,000 hadi 8,500 kwa jiji la Dar es Salaam.

Kilo ya mchele mzuri uliokuwa ukiuzwa Sh. 1,500 sasa umpenda hadi Sh. 2,500 huku unga wa ngano ukipanda kutoka Sh. 1,200 hadi Sh. 2,000.

Kupanda kwa bei hizo pia kunachangiwa na mavuno kutokuwa mazuri kwenye msimu uliopita kutokana na mabadiliko ya tabianchi, ambayo yamesababisha mvua kuwa kidogo.

Kwa ujumla gharama za maisha zimezidi kuongezeka na bei zinaongezeka kila kukicha kwenye kila bidhaa, jambo ambalo linawafanya watu kuhaha namna ya kuendesha familia kwa kipato walichonacho.

Bidhaa kwenye masoko zimeendelea kupanda na sasa ni vigumu kupata kitu kinachouzwa Sh. 500, vingi vinaanzia Sh.1,000 kwenda juu zikiwamo nyanya, vitunguu, bamia, hoho, karoti na ndizi.

Wakulima wameamua kuuza mazao kabla ya kuyavuna kwa kuwa wanunuzi kutoka maeneo mbalimbali wanafika bei, kiasi kwamba chakula kinakwenda kwenye masoko mengine na ya ndani yakikosa.

Serikali imeeleza jitihada mbalimbali ikiwamo kuwa na hifadhi ya chakula, lakini bado kuna tatizo la kufuatilia bei kwa kuwa wanufaika wakubwa ni mawakala ambao huwaulizia wachuuzi wa chini wanaouza sokoni.

Hali ya maisha ya mkulima inazidi kuwa mbaya kila siku na kubaki kufanya kilimo cha mazoea ambacho hakimkwamui kiuchumi, huku mchuuzi wa mwisho akibaki kuwa muuzaji mdogo mdogo asiyepiga hatua kubwa kimaisha.

Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alikaririwa akiahidi kutoa tamko la serikali Julai 15, mwaka huu.

Pia anakiri kuwapo upungufu wa uzalishaji msimu wa 2021/23 akiba ya msimu wa 2020/21 ikiisha, na kwamba mahitaji yameongezeka kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa kwa kuwa mvua zilikata zikaathiri mazao kukomaa.

Ni muhimu serikali ikaendeleza mkakati wa kuelimisha wananchi umuhimu wa kuhifadhi chakula, hasa wakulima kutoshawishika na bei wanazopewa kwa kuwa wakihifadhi watapata zaidi.

Pia ni muhimu kuhamisha na kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji ambacho hakiathiriwi na ukosefu wa mvua.

Ni muhimu kufundisha kuhifadhi na kusindika vyakula hasa msimu ambao kinazalishwa kwa wingi ili kusaidia kuwa na uhakika wa chakula hasa nyakati ambazo kuna uhaba.

Kwa sasa hali ni ngumu kwa kuwa watu hawana utamaduni wa kuhifadhi, hawajui njia bora za uhifadhi wa chakula na umuhimu wake, ndiyo maana kuna haja ya kutoa elimu sahihi kwa wakati sahihi.

Tanzania imejaliwa mikoa ambayo ni wazalishaji wakubwa wa chakula, ni muhimu wakulima wakaelimisha mbinu za kilimo bora kinachohimili hali ya hewa iliyopo.

Kwa na ufuatiliaji wa karibu wa shughuli za kilimo na kutoa ushauri wa mara kwa mara, pia kufuatilia kama ushauri unafanyiwa kazi ipasavyo.

Mwaka jana Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), walitoa tahadhari ya uwepo wa mvua chache na kushauri aina ya mazao ambayo hayahitaji mvua nyingi, lakini kwa kuwa hakukua na ufuatiliaji wakulima waliendelea kulima mazao yale yale na hawakupata mavuno.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mgongo wazi na vichwa vikubwa vinazuilika wanawake wakiamua

Na Jenifer Gilla

**HIVI** karibuni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa wito kwa wanawake walio kwenye umri wa kuzaa au wanaopanga kupata watoto kula vyakula vyenye kuongeza madini aina ya folic ili kuongeza kinga ya kumkinga mtoto kuzaliwa na mgongo wazi au kichwa kikubwa.

Waziri Ummy aliyasema hayo, aliposhiriki mbio za marathon zilizoandaliwa na Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), kwa ajili ya kuchangisha fedha za matibabu kwa watoto 200 wenye tatizo la kichwa kikubwa.

Alisema tatizo hilo linatokana na ukosefu wa madini ya 'Folic Acid', tatizo linaloweza kuzuilika, ikiwa wanawake walio tayari kuzaa wakitumia dawa hizo.

Taasisi mbalimbali za afya, ikiwamo Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) inaeleza mama mtarajiwa kutumia vidonge hivyo miezi mitatu kabla ya kubeba ujauzito na wiki 12 za mwanzo za ujauzito huo.

Kituo hicho kinaeleza ulazima huo unatokana na vidonge hivyo kusaidia kuzuia kasoro kubwa katika ukuwaji wa mtoto anapokuwa tumboni mpaka kuzaliwa.

> **Kwa mantiki hiyo, kama kinamama watarajiwa wasipotumia vidonge hivyo ndani ya kipindi muhimu kinachoelekezwa na wataalamu wa afya ndipo kunasababishwa kuzaliwa watoto wenye matatizo hayo.**

Kwa mantiki hiyo, kama kinamama watarajiwa wasipotumia vidonge hivyo ndani ya kipindi muhimu kinachoelekezwa na wataalamu wa afya ndipo kunasababishwa kuzaliwa watoto wenye matatizo hayo.

Hivyo basi, ili wazazi watarajiwa waweze kufuata maagizo hayo kwa umakini kuna haja ya wao kupanga uzazi kwa maana ya lini anatarajiwa kubeba ujauzito ili aweze kufuata utaratibu muhimu ikiwamo kumeza vidonge hivyo miezi mitatu kabla ya kupata ujauzito.

Ni wakati muafaka kwa wamama watarajiwa kuachana na dhana ya kubeba ujauzito kwa mazoea badala yake wakae na wenza wao na kuamua ni wakati gani wabebe ujauzito ili kufuata vizuri maelekezo ya wataalamu ya kumeza vidonge hivyo.

Daktari Bingwa kutoka Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Dk. Laurent Mchome, alisema kuwa taasisi hiyo inapokea watoto 700 hadi 1,200 wenye tatizo la vichwa vikubwa kwa mwezi na sababu kuu ikiwa ni lishe duni kwa wajawazito.

Dk. Laurent aliongeza kuwa kati ya watoto 100 wanauzaliwa, watoto watatu hadi wawili wana uwezekano wa kuzaliwa na mgongo wazi au kichwa maji.

Ukweli ni kwamba Tanzania tukiamua tunapunguza au kumaliza kabisa idadi hiyo inawezekana kwa kuwa mhusika mkuu ni mbeba mimba mwanamke akisaidiwa na mwenza wake hivyo watu hawa ni kiungo muhimu katika hatima ya mtoto anayezaliwa.

Lakini kuna hili kundi la pili la wanawake ambao hawapendi kutumia vidonge hivyo kwa sababu mbalimbali ikiwamo kuwa vinaharufu na ladha mbaya mdomoni. Dhana ambayo kama wanawake wasipoachana nayo itaongeza idadi ya watoto wanaozaliwa na ugonjwa huo.

Kama mwanamke, unaweza kuvumilia heka heka za mimba kama vile kichefuchefu, kuumwa kichwa, kutosikia hamu ya kula, kiungulia na kutapika kwa muda wa miezi tisa, hivi unashindwa nini kuvumilia harufu ya muda mfupi ya vidonge ambavyo vinakwenda kuokoa maisha ya mtoto wako?

Serikali inafanya juhudi kubwa kuzuia watoto wenye tatizo hilo kuzaliwa nchini, kwa kuboresha huduma ya uzazi hususani kabla, wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua ni jukumu letu kushirikiana nayo kwa kufuata miongozo yao na kutii maagizo yao ikiwamo hili la kutumia vidonge.

Wataalamu wa Afya na wadau wa uzazi salama wasichoke kuelimisha jamii kuhusu tatizo hili na namna linavyoweza kuzuilika ili kuiongezea nguvu serikali katika kufikia malengo ya utekelezaji wake na kuondoa kizazi tegemezi cha baadaye.



Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi (wa pili kushoto), akipewa ufafanuzi kuhusu huduma za WCF na mmoja wa maofisa wa mfuko huo wakati alipotembelea banda hilo akiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Dk. John Mduma (wa pili kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Elimu kwa Umma, Laura Kunenge. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yajivunia malengo kiutendaji ya WCF

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema inajivunia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), ulivyofikia malengo yaliyokusudiwa kwa kuongeza matumaini kwa wafanyakazi.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alitoa kauli hiyo alipotembeela banda la Mfuko huo kwenye Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), yaliyofikia kilele jana Julai juzi, 2022.

Mfuko huo ambao ulianza kutekeleza majukumu yake miaka sita iliyopita, unatoa fidia kwa mfanyakazi aliyeumia, kuugua na kufariki kutokana na kazi kwa mujibu wa mkataba na mwajiri wake.

"Sisi serikali tunaridhika sana na jinsi mnavyotekeleza majukumu yenu, mmewaondolea hofu wafanyakazi na sasa wanafanya kazi kwa kujiamini," alisema.

Alisema na waajiri nao wamepata fursa ya kujielekeza katika biashara na uzalishaji mali kwa kuwa ni kazi ya kumhudumia mfanyakazi anapopatwa na madhila yoyote akiwa kazini kama kuumia, kuugua na kufariki, WCF inachukua jukumu hilo.

"Tunaendelea kushuhudia, pamoja na kulipa fidia mfuko pia unatoa huduma ya utengamao na kuwasaidia wale ambao wamepata maumivu kwenye viungo vyao wanapatiwa matibabu na wakati mwingine wanapopona wanarudi kazini na kuendelea na majukumu yao," alifafanua.

Wakati huo huo, WCF umeibuka mshindi wa tatu kati ya wizara, wakala na taasisi zote za serikali zilizoshiriki kwenye Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Sabasaba 2022).

Ushindi huo umetangazwa wakati wa kilele cha maonesho hayo Julai 13, 2022 na mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Akizungumzia mafanikio hayo, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, aliwashukuru wadau waliotembelea banda la WCF.

"Tunawashukuru sana viongozi wa serikali pamoja na wadau wetu wote waliojitokeza kwa wingi sana mwaka huu kutembelea banda la WCF. Kwa pamoja tumeshinda," alisema Dk. Mduma.

# JKT yaongezea vifaa vya kisasa kampuni zake

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), limeendelea kuziimarisha kampuni zake tanzu zinazotoa huduma mbalimbali kwa kuzongezea vifaa vya kisasa likiwamo gari maalum la kusafirisha fedha ambalo litahudumia taasisi za fedha na kusafirisha madini migodini.

Vitendea kazi vingine vilivyonunuliwa ni gari la zimamoto, basi aina ya Toyota Coaster na pikipiki 16, vifaa vyote vimegharimu Sh. milioni 529.5.

Akizungumza jana baada ya kuzindua vitendea kazi hivyo, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa SUMAJKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele, alisema vifaa hivyo vitatumiwa na Kampuni ya Ulinzi ya Jeshi hilo SUMAJKT Guard na Kampuni ya usafi na Unyunyiziaji Dawa SUMAJKT.

Meja Jenerali alisema kampuni hizo zimeendelea kupata kazi na kuliongezea faida shirika.

"Magari tunayozindua leo ni kwa ajili ya kuimarisha kazi za ulinzi na usafi wa kila siku, azma ya SUMAJKT ni kuhakikisha miradi inakuwa na vitendea kazi vyenye ubora na vya kutosha ili zifanye kazi kwa ufanisi na tunataka ziende kwenye mitambo zaidi," alisema.

Alisema wameweza kuongeza idadi ya magari manne yenye thamani ya Sh. milioni 710.872 na pikipiki 16 zenye thamani ya Sh. milioni 41.6.

Aliwataka watendaji wote wa SUMAJKT kufanya kazi kwa bidii, weledi na ufanisi ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwa JKT na shirika hilo.

"Tukizingatia haya tutasaidia shughuli za uzalishaji mali na utekelezaji wa miradi kufanywa kwa wakati kwa ubora na tija jambo ambalo litasaidia shirika kupata miradi mingi na yenye tija. Kila mmoja wetu kwa nafasi yake ana jukumu la kuhakikisha anafanya bidii sehemu yake ya kazi. "Magari na pikipiki hizi zimenunuliwa kwa lengo la kuongeza mapato, wakati mwingine tunapokuwa na miradi mingi inatulazimu kukodi magari na vitendea kazi vingine kwa watu binafsi."

Meja Jenerali Mabele alisema ununuzi huo utasaidia kuondoa matatizo hayo ya ukodishaji na badala yake kuokoa kiasi cha fedha ambacho kingetumika kukodisha.

"Ninapenda kuona watendaji wote watakaopewa dhamana ya kutunza au kuvitumia vifaa hivi, wanavitumia kwa uangalifu na kuvitunza ili viongeze faida kwa JKT na shirika," alisema.

Aliwaeleza watendaji kuwa uzinduzi wa vifaa hivyo uongeze chachu na bidii zaidi katika utekelezaji wa miradi ya ulinzi, usafi na ujenzi.

Mwenyekiti wa Bodi ya SUMAJKT, Meja Jenerali Farah Mohamed (mstaafu), alitaka upanuzi wa huduma zinazotolewa na kampuni hizo uendane na kujizatiti ili wafanye kazi vizuri zaidi kuliko kuwa na watu na maeneo mengi ambayo hayaleti tija.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT, Kanali Petro Ngata, alisema shirika katika kutekeleza mkakati wake wa kuongeza vyanzo vipya vya mapato na kuboresha huduma na bidhaa, limepanga kununua vitendea kazi vipya kadri hali ya fedha itakavyokuwa ikiruhusu.

Alisema vitendea kazi hivyo, vitaongeza ufanisi katika utendaji kazi wa kampuni zake tanzu kwa kupunguza matatizo yaliyokuwa yakijitokeza kutokana na upungufu wa vifaa.

Pia alisema vitaongeza wigo wa mapato kwa kuongeza njia nyingine za uzalishaji.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa SUMAJKT Guard, Joseph Masanja, alisema kwa sasa kampuni hiyo ina jumla ya watendaji 14,839 na kati ya hao, wanaume ni 10,857 na wanawake ni 3,982 wanaotoa huduma ya ulinzi nchini.

Alisema kwa sasa magari ambayo kampuni hiyo itakuwa nayo yakiwamo yaliyozinduliwa jana ni 49, pikipiki 134, mitambo na mashine zitatumika katika shughuli za operesheni na utawala.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Usafi na Unyunyiziaji dawa SUMAJKT, Kapteni Rosemary Katani, alisema wanatekeleza shughuli zao katika mikoa 12 iliyopo Tanzania Bara na ina jumla ya wafanyakazi 1,500.

Alisema kampuni imenunua gari la kisasa la taka lenye thamani ya Sh. milioni 222.9 na uwezo wake ni kuchakata na linabeba takataka nyingi kwa mara moja na kuzihifadhi bila kutoa harufu na zenye majimaji zina eneo lake maalum.

# Wamiliki maeneo ya kazi watakiwa kuyasajili OSHA

**Frank Monyo**

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amewataka wamiliki wote wa maeneo ya kazi kuhakikisha wanasajili maeneo yao ya kazi na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) ili taasisi hiyo iweze kuwafikia na kuwapa huduma za ukaguzi na ushauri kuhusu usalama na afya mahali pa kazi.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kuhitimisha ziara katika taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ikiwamo OSHA zilizokuwa zinashiriki Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba).

"Suala la msingi zaidi ninalolisisitiza hapa ni kwa wamiliki wa sehemu za kazi ama waajiri kuendelea kujisajili katika Taasisi ya OSHA ili waweze kufanyiwa ukaguzi wa maeneo yao ya kazi katika kutekeleza Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi.

"Ni wajibu wa serikali na waajiri wote kuhakikisha maeneo yote ya kazi yanakuwa salama na kazi zinazofanyika zinakuwa zenye staha na suala hilo linaanza na kuwa na afya njema kwani afya ndio mtaji namba moja katika uzalishaji," alisema Katambi na kuongeza:

"OSHA wamekuwa wakiendelea kusimamia kazi hii vizuri na kuhakikisha wakati wote wanatembelea maeneo ya kazi kwa ajili ya kufanya ukaguzi ili kutambua maeneo hatarishi na kutoa maelekezo na miongozo ya namna sahihi za kuwakinga wafanyakazi kwa mujibu wa sheria na kuwachukulia hatua stahiki wale wanaokaidi maelekezo ya serikali."

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema jukumu kuu la taasisi yake ni kuwezesha biashara na shughuli mbalimbali za uwekezaji nchini ili shughuli hizo ziweze kuwa na tija.

"OSHA ni taasisi wezeshi na kama inavyofahamika dhamira ya serikali ya awamu ya sita ni kuhakikisha kwamba inakuza biashara na uwekezaji nchini hivyo sisi tumeangalia nini tunaweza kufanya katika kufanikisha dhamira ya serikali na tukaona tuondoe tozo takribani 13 zenye thamani ya zaidi ya bilioni 35 ambazo kama zingeingia katika mfuko mkuu wa serikali zingeenda kujenga barabara, shule hospitali, lakini Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia fedha hizi kubakia mikononi mwa wawekezaji ili zikaboreshe mifumo ya kuwalinda wafanyakazi," alisema Mwenda.

## Nape: Mazingira ya habari kuboreshwa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amewahakikishia washirika wa maendeleo kuwa, serikali inaendelea kuboresha mazingira ya wanahabari na upatikanaji wa taarifa katika mazingira yote.

Pia amesema serikali inatambua mchango wao katika sekta ya habari nchini.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano uliokutanisha pamoja washirika wa maendeleo na serikali ukilenga kupitia na kuangalia hali uhuru wa habari nchini na upatikanaji wake.

Mkutano huo uliongozwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) na Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN).

Katika mkutano huo pia walijadili namna teknolojia inavyosaidia upashaji wa habari, mazungumzo ya uhuru na mazingira ya wanahabari katika kufanya kazi vizuri.

Akifungua mkutano huo, Waziri Nape alisema serikali inatambua mchango wa wadau wa maendeleo katika kusaidia ukuaji wa vyombo vya habari nchini.

"Tunatambua mchango wao katika upashanaji habari, matumizi ya teknolojia katika nchi yetu, pili tumeendelea kusisitiza wajibu wa serikali inayoongozwa na Rais Samia, kuhakikisha tunaendelea kuboresha mazingira ya wanahabari na upatikanaji wa taarifa katika mazingira yote.

"Mchakato wa kupitia sheria na kanuni unaendelea vizuri lakini tunapitia na sera ya habari, hapa ni mambo matatu kwa pamoja, ninaona wengi wanazungumzia zaidi sheria lakini sheria inatengenezwa na sera, sera inatengeneza sheria na sheria inatengeneza kanuni."

Waziri Nape aliwashukuru wadau wa maendeleo kwa namna ambavyo wanashiriki katika kujadiliana na kubadilishana mawazo na kuona namna wanaifanya sekta na nchi iendeleee zaidi.

Waziri Nape alisisitiza kuwa bado wizara yake ipo kwenye majadiliano na wadau wanafurahia kwa sababu walipeleka mawazo yao na serikali imetoa yake na kwa pamoja wakajadiliana.

"Tumezungumza tujue namna ya kuboresha, nimewahi kusema na hapa naomba nirudie, sheria ya habari ilipotungwa ililenga kutatua matatizo katika sekta ya habari, ikiwamo matatizo ya ajira zao, maslahi, mazingira yao ya kazi, haki zao na wajibu wao.

"Inawezekana masuluhisho yaliyowekwa kwenye sheria ndiyo yanayogombaniwa kwamba ni sahihi au siyo sahihi, katika mazingira hayo serikali imetoa nafasi kwa wanahabari kuleta mbadala kwa yale yanayolalamikiwa tukae mezani tuzungumze na huo mchakato hauwezi kuwa mfupi.

"Nimeukuta tunaendelea nao na malengo ya kuukamilisha mapema kadri inavyowezekana tutakapokubaliana tutaukamilisha. Lengo tutunge sheria itakayokaa muda mrefu, itakayokubalika kwa pande zote mbili, itakayotengeneza mazingira yawe bora zaidi kuliko tuliyonayo, hilo ndiyo kubwa," alisema.

# DC awahimiza waandishi kutetea haki za binadamu

**Na Beatrice Shayo,**
MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, amewataka waandishi wa habari kuacha kuandika habari zenye uchochezi kwa kuwa zinachangia uvunjifu wa haki za binadamu.

Msando aliyasema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa wanahabari kuhusu namna bora ya kutoa habari hasa zinazohusu haki za binadamu, katika mkutano ulioandaliwa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THDRC). Alisema habari za ushabiki hazina tija katika jamii kwa sababu zinachangia kuvunja haki za binadamu.

"Teteeni haki za binadamu. Tuko katika mazingira ambayo kwa sasa ni salama zaidi katika kipindi chote duniani zamani nchi zinapata uhuru na nchi kupambana kimaendeleo waandishi wa habari uhuru wao ulibanwa, lakini sheria zetu zilizotungwa na za kimataifa zinatoa uhuru kwa waandishi wa habari," alisema.

Masando alisema hakuna sababu ya kuishi kwa hofu na woga wakati wa kutekeleza majukumu yao ya uandishi wa habari.

Pia alisema serikali ya awamu ya sita inawahakikishia waandishi wa habari haina nia wala sababu yoyote ya kuwanyima uhuru wao, na kwamba wanatakiwa kufanyakazi kwa uhuru kwa kuandika kweli kwa kuzingatia maadili ya taaluma yao.

"Ondokeni kwenye 'hangover' ya vipindi vilivyopita huko nyuma ya kusifia sana au kupinga sana kuna baadhi ya waandishi wana hiyo 'hangover' anashindwa kuelewa sio lazima kusifia sana ama kupinga sana unatakiwa kufanya kazi yako ya uandishi wa habari kwa kuripoti ukweli na haki," alisema.

Msando alisema kwenye haki za binadamu sio lazima kuandika tu zinapovunjwa ziandikwe hata pale zinapokuwa hazivunjwi.

Alisema inapotokea mahakama imefanya vizuri ikiwamo kumaliza kesi ndani ya muda uliopangwa itafutwe hiyo taarifa na kuandikwa ili jamii ijue mahakama imefanya hivyo.

"Mfano jaji wetu hapa Morogoro anafanya kazi nzuri anapunguza kesi na misongamano anatoa adhabu mbadala, ikiwamo adhabu ya kupanda miti ili kulinda mazingira taarifa kama hiyo huwezi kuisikia kwenye vyombo vyetu vya habari," alisema Msando.

Naye Jaji Mstaafu Robert Makaramba akiwasilisha mada ya wanahabari namna ya kuandika na kuripoti habari za mahakama, alisema ni muhimu kuepuka kutoa taarifa ambazo hazijatolewa mahakamani ili kuepuka kujiingiza kwenye migogoro.

Awali, Wakili wa THRDC, Leopold Mosha, alisema mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo waandishi wa habari namna ya kuripoti taarifa zinazohusiana na haki za binadamu.




Mwenyekiti wa Bodi wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Meja Jenerali mstaafu Michael Isamuhyo (wapili kulia) na Mkurugenzi wa STAMICO, Dk. Venance Mwesse (kushoto), wakiwa pamoja na Meneja Uhusiano na Masuala ya Ndani wa Barrick, Neema Ndossi na Mratibu wa Uhusiano na Masuala ya Ndani wa kampuni hiyo, Abella Mutiganzi, baada ya kampuni hiyo kukabidhiwa tuzo za ushindi za TANTRADE, wakati wa kufunga maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa Dar es Salaam juzi. Barrick ilishinda tuzo za kuongoza kuuza madini katika migodi yake ya Bulyanhulu na North Mara na mwasilishaji bora wa michango ya wafanyakazi kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maofisa wanolewa sheria za mbegu

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

MAOFISA kilimo, mipango na wanasheria wa halmashauri za mikoa ya Kanda ya Kaskazini, wamepewa elimu kuhusu mabadiliko ya sheria za mbegu.

Meneja wa Sera wa Kituo cha Kuendeleza Kilimo, Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), Khalid Mgalamo, alitoa mafunzo hayo yaliyohusisha maofisa 80 kutoka halmashauri 20 za mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Morogoro.

Semina hiyo pia ilihusisha Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa ufadhili wa Taasisi ya Mapinduzi ya Kijani barani Afrika (AGRA).

Alisema lengo la semina hiyo ni kuwajengea uwezo watendaji wa halmashauri juu ya mabadiliko yaliyofanyika ngazi ya taifa, ili sheria ndogo wanapoziandaa zisitofautiane au kukinzana na mabadiliko yaliyopo.

"Semina hii imefanyika kwenye mikoa ambayo inamazingira wezeshi ya uzalishaji wa mbegu na nia yetu ni kuwajengea uelewa wa mabadiliko ya sheria za mbegu na tozo mbalimbali yaliyofanyika katika ngazi ya taifa ili sekta ndogo ya mbegu iendelee kuimarika," alisema.

Pia alisema tozo za mbegu zilizowekwa na halmashauri zote imeondolewa katika mwaka wa fedha wa 2022/23, ili kuondoa mgongano kati watendaji wa halmashauri na wazalishaji wa mbegu.

"Kupitia semina hii tunatoa ujumbe kwamba uaandaji wa sheria ndogo katika halmashauri lazima uzingatie maboresho ya sheria na sera yaliyofanyika katika ngazi ya taifa, jambo litakalosaidia kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu nchini," alisisitiza Mgalamo.

Naye Mkuu wa Uratibu wa Sekta za Uchumi na Uzalishaji wa TAMISEMI, Leo Mavika, alisema semina hiyo imekuja wakati mwafaka kwa sababu kuna mabadiliko mengi ya sheria ngazi ya taifa kuhusu tozo na kodi mbalimbali hususani za mbegu na kwamba itasaidia kuwajengea uelewa watendaji juu ya mabadiliko hayo.

"Ofisi ya Rais TAMISEMI ndio watekelezaji wa sheria, sera, miongozo na kanuni mbalimbali. Lengo la semina hii ni kuboresha mazingira ya kufanya uzalishaji wa mbegu na usimamizi na utungaji mzuri wa sheria ndogo," alisema Mavika.

Awali Ofisa Miradi wa AGRA, Ipyana Mwakasaka, alisema semina hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa kuboresha sheria na sera za mbegu ili kuongeza uzalishaji, ili Tanzania iweze kujitegemea kwa mbegu na hata kuuza nje ya nchi.

"AGRA itaendelea kushirikiana na serikali na wadau wengine katika sekta ya kilimo ili kuhakikisha sekta ndogo ya mbegu inaboreshwa kwa kuzalishaji mbegu bora na mbegu kumfikia mkulima kwa gharama nafuu jambo litakaloongeza uzalishaji wa mazao nchini," alisema Mwakasaka.

# RC apiga mafuruku magari 'mchomoko'

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amepiga marufuku usafiri wa magari ya abiria, maarufu michomoko, yanayotumika kusafirishia abiria kutoka mji wa Bariadi kwenda maeneo tofauti tofauti.

Kiongozi huyo alifikia uamuzi huo jana kutokana na ajali iliyotokea usiku wa kuamkia juzi, nje kidogo ya mji wa Bariadi, iliyosababisha vifo vya watu watano na wengine 11 kujeruhiwa.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukutana na kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa, Kafulila alisema vyombo hivyo vya usafiri pamoja na wamiliki wake hawafuati maelekezo ya serikali, ikiwamo Mamlaka ya Udhibiti Usafirishaji wa Ardhini (LATRA).

Kafulila alisema pamoja na hatua nyingine za kiutawala zinazoendelea kutokana na ajali hizo, amefikia uamuzi huo kwa magari hayo yanayobeba abiria.

Alisema ili gari lifanye kazi kama daladala, kuna utaratibu wake ikiwamo kuwa na rangi, alama na namba, ili likitokea jambo lolote iwe rahisi kuratibu na kufahamika.

"Wamiliki na waendeshaji wa michomoko kwa zaidi ya nusu mwaka wameshapewa maelekezo ya taratibu za kufuata ili waendelee na kazi, lakini hadi sasa hakuna gari iliyotekeleza maelekezo ili isajiliwe," alibainisha.

Kafulila alisema ajali zinagharimu maisha ya watu kwa kusababisha na wengine kupoteza maisha, huku taifa likipata hasara ya nguvu kazi.

Aidha, alitoa wito kwa wamiliki wa magari ya abiria na wawekezaji wa sekta ya usafirishaji kuwekeza mkoani humo kwa kwua abiria ni wengi.

Kwa upande wake, Ofisa Mfawidhi wa LATRA mkoani Simiyu, Amaniel Sekulu, alisema kuna ukiukwaji wa sheria utumiaji wa vyombo vya usafiri maarufu kama michomoko, ambavyo vinapewa leseni ya usafirishaji wa abiria kama daladala na inawapasa kubeba abiria wanaoenda na uwezo wake na sio kufanya kazi kama daladala.

Alisema vyombo hivyo vinatakiwa kusajiliwa, kupakwa rangi za utambulisho, kuwa na namba ya utambulisho pamoja na kibao cha kuonyeshwa ni tax kwa upande wa juu, ili kijulikane kuwa ni chombo cha usafiri.

"Kwa muda mrefu sasa tangu vipewe leseni havijatekeleza masharti hayo ambayo serikali iliyatoa, kutokana na ajali ambazo zimetokea na shida ambazo Watanzania wanazipata serikali ya mkoa wa Simiyu imeamua kuzuia aina hii ya usafirishaji.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kulia), akikabidhi tuzo ya ushindi wa kwanza wa sekta ya mawasiliano kwa Mkurugenzi wa Dijitali na Huduma za Ziada wa Vodacom Tanzania Plc, Nguvu Kamando, baada ya kampuni hiyo kuibuka kidedea katika maonesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam yaliyomalizika juzi. Kushoto ni Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ubovu barabara wakwamisha ufuta kufika sokoni kwa wakati

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

BAADHI ya wakulima wa ufuta wameshindwa kufikisha mazao yao kwenye maghala na kushiriki minada inayoendelea kutokana na ubovu wa barabara kutoka mashambani, imeelezwa.

Hayo yalisema jana na Husein Mohamed kutoka kampuni ya usafirishaji ya Tinge iliyoko wilayani hapa inayosafirisha ufuta wa wakulima kutoka shambani hadi kwenye maghala.

Mohamed alisema wako wakulima ambao hadi sasa wamekwama kufikisha ufuta kwenye kutoka kwenye mashamba hadi kwenye maghala kutokana na hali ya usafiri na ubovu wa barabara ambao unakwamisha magari kufika kwenye maeneo husika.

"Katika maeneo ya Ruaruke na Makima barabara ni mbovu. Magari yakienda huko yanaharibika na wasafirishaji wengine wanakwepa kwenda kutokana na kuhofia kuharibu magari," alisema.

Kwa mujibu wa Mohamed, hali hiyo imesababisha baadhi ya wakulima kushindwa kushiriki minada na ufuta wa kutofika kwenye maghala kwa wakati.

Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Pwani (CORECU), Mantawela Hamisi, akiwa kwenye mnada wa ufuta, alisema hadi sasa wako wakulima ambao hawajafikisha ufuta kwenye maghala wengine wakidaiwa kusubiri bei zipande.

Mantawela alisema katika mnada uliofanyika juzi Kibiti wanunuzi wamepungua kutoka zaidi ya 20 waliokuwa wakijitokeza hadi watatu lakini bei imepungua kutoka Sh. 3,090 hadi Sh. 3,026 kwa kilo.

Meneja huyo alisema kuendelea kupungua kwa wanunuzi inaonyesha minada ya ufuta inaendelea kufungwa hivyo ni vema wakulima wenye ufuta wakapelekea kiasi walichonacho kwenye maghala kuepuka hasara ambayo wanaweza kuipata kwa kuuza kwa mtu mmoja.

CORECU inatarajia kufanya mnada wa mwisho wa ufuta wiki ijayo kwa ajili ya kutoa muda wakulima kuendelea na maandalizi ya zao la korosho kwa kufanya usafi na kupulizia dawa kulingana na taratibu za kilimo hicho.

# Wanunua eneo kujenga shule

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MGODI wa Mwime ulioko Kata ya Zongomela Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, chini ya Umoja wa Kikundi cha Wamiliki wa Mashamba (KABELA), wamenunua ekari tano kwa thamani ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya msingi.

Kikundi hicho kimefikia uamuzi huo baada ya kuona Shule ya Msingi Ilindi ya Mtaa wa Mwime kuwa na wanafunzi zaidi ya 2,000 ambao wanasoma kwa shida.

Meneja wa KABELA, Joseph Nalimi, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea mgodi huo ili kujionea hali halisi ya maendeleo ya mtaa huo ambao una mgodi.

"Baada ya kukaa na serikali ya mtaa huu, tuliona kwenye suala la elimu shule yetu ya msingi imezidiwa sana na wanafunzi. Tumejaribu kuwa tunajenga madarasa pale lakini hayawezi kutosha na tukabaini kuwa hata tukijenga madarasa 50 bado mwalimu mkuu atakuwa na mzigo mzito," alisema.

"Tuliona dawa ni kujenga shule mpya. Kwa maana hiyo, tukaomba mpango kazi ambapo mgodi tukalinunua eneo kwa gharama ya Sh. milioni 10 tukalikabidhi kijiji na hati wanayo, wakampa taarifa mkurugenzi wa halmashauri ya manispaa ambaye aliwapa Sh. milioni 120 za madarasa sita," alisema.

Meneja huyo alisema mgodi utajenga madarasa mawili ili kuongeza pamoja na ofisi mbili za walimu na wakachimba karo na kujenga boma la choo matundu 12 yakiwamo sita ya wasichana na sita wavulana na kwamba tayari wamemkabidhi mkurugenzi kwa ajili ya umaliziaji.

Meneja huyo pia alisema waliamua kujenga choo cha walimu matundu mawili na kukarabati ofisi ya kijiji kwa kuezua paa na kuanza kujenga upya mpaka rangi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Ilindi, Dogo Mheziwa, alipongeza mgodi huo kupitia kikundi cha umoja wa wamiliki wa mashamba kusaidia shughuli mbalimbali za maendeleo kwa wananchi wake, na kwamba manispaa imetoa Sh. milioni 120 za kumalizia shule ya msingi Mwime.

Ukurasa 13




Hii inawezekana kwa magereza yetu Bongo?

BUFE
IJUMAA JULAI 15, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



**'Kuupiga mwingi' kwa Rais kulivyoibua kicheko cha walima korosho wa Mtwara**

Ukurasa 12


# Kijana Protasi, apambana na hali kwa juisi miwa 'maisha yaendelee'Mwanza

**Na Anthony Gervas, Mwanza.**

MIWA inajulikana kuwa zao la biashara na chakula, nikimaanisha linaweza kuzalishwa sukari na juisi viwandani. Kuna imani ya kiafya kwa watu wengi kwamba mtu akila miwa, inasaidia kusafisha figo na kuongeza sukari mwilini.

Zao hilo, ni sehemu kubwa ya uchumi wa pato la taifa ambalo hulimwa kwa wingi katika mikoa mbalimbali nchini kama vile Morogoro, Kagera na kwingineko.

Katika jiji la Mwanza Nipashe iliingia mtaani na kukutana na kijana mmoja ambaye anafanya biashara ya kuuza juisi ya miwa mtaa wa Kaluta, hata kupata fursa ya kumdadisi namna anavyonufaika nalo, katika kijiwe chake amejiegesha kwenye ukuta wa uchochoro katika nyumba mojawapo.



Kijana Melitus Protas, akiwa kazini anakamua juisi ya miwa kwenye mashine aliyopewa kwa mkataba. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

"Ninafanya biashara, nauza juisi ya miwa kwa mkataba wa mwaka mmoja, baada ya tajiri kunipa mashine ya kukamulia, tumefunga mkataba kila wiki nampelekea shilingi 28, 000," anasema Melitus Protas.

Anabainisha kwamba, pale mkataba unapoisha, mashine aliyokabidhiwa na tajiri huyo kutumia inakuwa mali yake anamiliki.

Protas (23) mkazi wa Isamilo jijini Mwanza, anasema akaamua kupambana kusaka maisha yake kwa kufanya kazi hiyo katika mtaa wa Kaluta akiwa na uzoefu wa miaka mitatu, kutoka alikotumikia.

Anasema amesoma katika Shule ya Msingi Nyakahama, iliyoko wilayani Muleba mkoa wa Kagera hadi darasa la saba na baada ya kuhitimu, aliamua kutoendelea na masomo ya sekondari, akajikita katika kufanya kazi ya kuvua samaki katika Ziwa Victoria, ambako ni jirani na kwao.

Protas akaamua kuacha uvuvi, kutokana na mjumuiko ambao haukumfurahisha kutoka kwa wavuvi, baadhi wakiwa watumiaji dawa za kulevya, bhangi na ulevi wa pombe, huku lingine la kero ni namna wavuvi wanavyotoa lugha chafu kwa watu, wakiwa mbali na staha, hawa wote wanaonekana wamekosa maadili mbele ya jamii.

Protas anasema kuna wakati amewahi kufanya biashara ya kuuza kahawa vijiweni katika mtaa wa Uhuru, jijini Mwanza, hata hivyo akashindwa akiiona kazi hiyo 'haimlipi' anavyotaka, kwa siku amekuwa akiambulia kuanzia Sh. 3,000 hadi Sh. 4,000 na kuna wakati anaishia kula huku akiwa amekosa faida stahiki.

Anasimulia mapito magumu kwake, kwamba ameshawahi kuelemewa gharama za mahitaji yanazidi faida aliyokusudia, anaponunua sukari, kahawa, mkaa na tangawizi.

Vilevile anasimulia mapito yake, kwamba hakuishia hapo baada ya kuachana na uuzaji kahawa mitaani, akaendelea kusaka maisha hadi akajiunga mafunzo ya ufundi stadi wa kupaka rangi za nyumba, ambazo amedumu takribani miezi miwili, nako akakuona kugumu, akaachana nayo.

Baadaye akafikia hatua kufanya shughuli nyingine ya kukamua juisi ya miwa, ambayo hadi sasa amedumu nayo kwa muda wa miaka mitatu.

Kijana huyo anasimulia, eneo anakofanyia biashara yake huwa analipa kodi ya Sh. 30,000 kwa mwezi, ikiwa ni wastani wa Sh.1,000 kila siku, huku bidhaa yake juisi ya miwa anauza kwa bei kila glasi ni Sh. 500.

Hapo analalama kwamba wao wafanyabiashara wadogo na hata wenzao wakubwa wanalia kutokana na kukosa wateja, ambayo inachangiwa na hali ngumu ya maisha.

Protasi anawataja wateja wake ni wapita njia na wafanyabiashara wenye maduka ya bidhaa jirani, bado analalamika, kuna wakati biashara yao inadorora sana, vivyo hivyo analalamika namna wakati mwingine anakumbwa na misukosuko ya mgambo wa jiji wanaotaka kuwaondoa kwa uchafuzi wa mazingira.

Kwa mujibu wa Protasi, miwa ya kukamua juisi huwa anapata kutoka shambani ,akitaja ameanza na mtaji Sh. 25,000, baada ya kuingia makubaliano na aliyekuwa mwajiri wake kumpa mashine kwa mkataba huo.

Ugumu mwingine anautaja, ni kwa wateja wanaokopa na kuchelewesha kurejesha fedha madeni ambayo ndiyo mzizi wa mtaji wa kuendesha biashara hiyo. Anaeleza kuwa malengo aliyo nayo sasa, ni kuhakikisha anamiliki mashine zake mbili za kukamua juisi ya miwa, moja akiajiri mtumishi na nyingine anaifanyia kazi mwenyewe.

Hapo mwana – Muleba huyo, aliyetua jijini Mwanza, anaanika lengo lake ni kujenga nyumba ya kuishi na familia jijini humo, hata akaondokana na kero za upangaji ambao anautaja ni 'pasua kichwa' pale anapochelewa kumlipa mwenye nyumba kodi yake.

Ana rai yake kwa vijana walioosoma, wote wanatakiwa kupambana kutafuta maisha, kwa kujiajiri baada ya kudumisha ndoto ya ajira, ambazo ni adimu.

Pia, ana kauli ya kukemea matumuzi ya kilichomkera kwenye uvuvi katika suala la dawa za kulevya kama vile bangi, mirungi na ulevi usiokuwa na tija maishani.

BIASHARA

# 'Kuupiga mwingi' kwa Rais kulivy kicheko cha walima korosho wa M

## •Ruzuku pembejeo shambani kupitia 'shotikati' bandari yao

**Na Halfani Chusi, aliyekuwa Mtwara**



Shamba la korosho likiwa tayari limesafishwa, kwa mujibu wa kanuni za kilimo, mmiliki akilihudumua.

NI wastani wa wiki tatu au zaidi, nilikuwa mahali ambako si mbali na mji wa Mtwara. Hapo nikiwa na baadhi ya wenzangu tunakaribia maeneo ya shamba la mkulima mmoja na kumkuta anapalilia shamba lake la korosho, huku akizama katika nyimbo zake za kabila la kimakonde, nami navutiwa na kuamua kutumia uanahabari wangu kumdadisi sababu ya bashasha hiyo?

Mkulima huyo anayejitambulisha kwa jina Saidi Abdallah, kutoka kata ya Magengeni, Mtaa wa Mkundi katika Barabara ya Nannela, katika Manispaa ya Mtwara, anabainisha anavyoguswa na kazi ya serikali katika zao lake la korosho.

Hapo anaendelea: "Tangu aingie huyu Rais (Samia) madarakani tumekuwa tukipewa ruzuku, pamoja na pembejeo za kilimo, kitu ambacho miaka ya nyuma hakikuwepo na wakulima tulikuwa tunashindwa kumudu gharama za kilimo na wengine walishindwa kuendelea na biashara hiyo kabisa.

"Kwa hiyo naweza nikasema Rais 'anaupiga mwingi', lakini kwa upande wa korosho huku Mtwara goli bado hajaliona na goli ni "kutufungulia viwanda vya kubangua korosho pamoja na kutuwekea benki rafiki kwa wakulima wa korosho, kwa kufanya hivyo atakuwa ameliona goli na kufunga na sisi tutaendelea kuzalisha korosho kwa wingi na kupata mazao yaliyo bora," anasema.

Ni aina ya kauli inayopokewa na mkulima mwingine mkoani humo kutoka Manispaa ya Mtwara Mkindani Mjini, Mtaa wa Pachoto B, Rashidi Mamkunda, naye anaambatanisha sifa kama za mtangulizi wake, akiunganisha ombi kwa Wizara ya Kilimo, kuhakikisha dawa zinafikia wakulima kwa wakati, ili kuepusha mimea kushindwa kumea vizuri kwa kisingizio cha dawa kuchelewa.

**CHAMA CHA WAKULIMA**

Meneja Mkuu Chama Kikuu Cha Ushirika Masasi Mtwara (MAMCU), Hadija Matipa, anabainisha kuwa tangu serikali ilipoanza kutoa ruzuku kwa wakulima, kumekuwapo matokeo chanya kwa wakulima.

"Nianze kwa kuishukuru serikali kwa kutujali sisi wakulima wa korosho. Kwa hiyo, utaona mabadiliko tangu tuanze kupata ruzuku msimu uliopita 2020-2021. Tulipata tani elfu 65.

"Pia, (mwaka) 2021-2022 tukapata tani elfu 69, lakini kwa mwaka huu kupitia Waziri wa Kilimo Hussein Bashe, tumeletewa pembejeo za kilimo kwa wakati. Kwa hiyo, dalili ni nzuri hivyo mwaka huu tunatarajia kupata tani elfu 85," anafafanua.

Mwenyekiti, Aloyce Mwanjire, pia Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania, Francis Alfred, wanaonyesha kukunwa na hatua ya Rais Samia kutoa viuatilifu bure kwa wakulima, ili waweze kutibu mazao yao.

Katika ufafanuzi wao wanasema kwa sasa wakulima wa korosho wanapokea dawa za Salfa ya unga, hii ni ili kutibu magonjwa ya korosho, hali wanayoiona kwamba itawapanulia uzalishaji korosho na kuwapa kipato kikubwa.

Rai yao wakuu hao wa Bodi ya Korosho, ni kwamba wakulima wa korosho waache kubweteka na misaada inayotolewa na serikali, badala yake wanawasisitiza wanapovuna mazao yao, wakumbuke kutenga pesa kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo.

**RC ATOA MAAGIZO**

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marko Gaguti , anaagiza watu wote watakaohusika katika ugawaji pembejeo hizo, wafanye hivyo kwa wakati na pasipo upendeleo, ili kila mkulima afaidike na pembejeo hizo.

"Namhakikishia Rais wetu mpendwa, pembejeo hizo zimefika mahali pake. Wakulima wa zao hili wamefurahi sana kuona ametoa tani 5,623 kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa zao la korosho.

"Kwa hiyo, nataka niseme wale wote watakaopewa nafasi ya kugawa pembejeo hizi, wakazigawe kwa umakini mkubwa, hatutasita kumchukulia mtu hatua pale tutakapobaini hali ya ubadhirifu katika pembejeo hizo," anatamka Brigedia Gaguti.

Pia, anarejea kwamba mwaka uliopita aliwachukulia hatua za kisheria wafanyakazi 12, wak-



Korosho ikiwa tayari mtini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# yoibua Mtwara

iwemo waajiriwa wa serikali kwa kosa la ubadhirifu kwenye pembejeo hizo za kilimo na akatoa msisitizo, kwamba hataki kuona hilo linajitokeza tena.

**KINACHOWAGUSA WAKULIMA**

Kwanini walima korosho wa Mtwara wanadumu kumsifu Rais Samia? Msingi wake unaanzia katika hatua yake kuwasaidia wakulima hao na kuwapatia pembejeo za kilimo, baadhi za bure wakulima wa korosho.

Hapo ujumla wake, unajumuisha dawa za kukuza na kustawisha mimea, hali inayotajwa kuwaongezea kipato wananchi kwa asilimia kubwa, Nipashe ikishuhudia hivi karibuni jumla ya tani 5,623 za pembejeo zikiingizwa nchini.

Pili, kuna linalotajwa la kufanyiwa marekebisho katika Bandari ya Mtwara, ili kuwarahisishia wakulima waliopo mkoani humo, pamoja na viongozi wa bodi ya korosho waweze kupokelea baadhi ya pembejeo za msaada kutoka serikalini kupitia bandari ya Mtwara na sasa kukishuhudiwa bandari hiyo inafanya kazi, meli kubwa zinawasili hapo kupakua na kupakia mizigo ya Kusini.

Tatu, ni msaada wa pembejeo za kilimo ambao Rais amewapa walima korosho kitaifa. Hapo ikimaanisha mikoa kama Pwani, Lindi na Ruvuma mahsusi katika wilaya ya Tunduru.

Kupitia mantiki hiyo, serikali inaendelea katika mikakati ya kufufua viwanda vya korosho vilivyokufa, ili suala la ubanguaji kitaifa ikiaminika kibiashara, zao hilo litaongezewa thamani ndani ya nchi na kuuzwa kwa bei ya juu ughaibuni, faida kubwa ya mnyoyoro wa thamani ikibaki nchini.

**CHANGAMOTO WALIZO NAZO**

Moja ya changamoto mbazo zinaendelea kuwaandama wananchi hao ni kukosa benki kwa ajili ya mikopo kwa wakulima, pia bado wanalia na bei ya mauzo ya zao lao.

Mengine wanayataja kuwa ni urasimu kwa baadhi ya viongozi wanaosimamia uzalishaji korosho, pale zinapoingia dawa na pembejeo za kilimo ambazo haziwafikii wakulima kwa wakati.

Lingine ni lialoendana na upungufu wa maofisa ugani wa kilimo, wanaoelezwa idadi yao haitoshi kuhudumia wakulima wote wa korosho. Hao wanahitimisha madai, kwamba serikali iweke mazingira bora kuwa ma benki inayowawezesha kukidhi maslahi yao ya shambani.

- ***Mwandishi anapatikana kupitia simu:+255 787879707***



Miche bora ya korosho, kwa ajili ya kuwapatia wakulima.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Hii inawezekana kwa magereza yetu Bongo?






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

JUZI kati hapa niko mtaani, sina hili wala lile, naingia chochoro fulani hivi, mara mbele yangu anatokea mwanamama ananiangalia na kisha ananishika mkono na kujisemea, enhee afadhali.

Namshangaa, ananiambia hebu tusogee huku, tunatoka kwenye chochoro na kuniambia hunijui, lakini mimi nakujua.

Wakati naendelea kushangaa, ananiambia nimesoma atiko (article) yako kwenye Nipashe. Umeandika kuhusu wafungwa, ukizungumzia mpango wa kulipwa posho na ukaonekana kuupinga, ukisema mfungwa ni mfungwa tu na kwamba hastahili hayo malipo. Sasa nataka tuzungumzie hilo.

Mwanzoni nilishaingiwa na hofu, kuwa huenda huyu atakuwa 'panya road' au 'panya kalewa', lakini nikaona ana nia njema ya kutaka tuelimishane, na hata akitaka kunizingua tuzinguane tu. Ndiyo sababu nikamkubalia mazungumzo.

Tulikuwa tumesimama, nikamsihi tutafute mahali pembeni tukae, kwani nilishamwona ana mazungumzo marefu. Jirani kulikuwa na kigogo tukakikalia, tukaendelea na mazungumzo yetu.

Akaniuliza, hivi mtoto akiwa tumboni mwa mama yake anakuwa mhalifu? Nikamjibu, hapana. Kwanini? Nikamwambia, atakuwa hajui lolote mpaka anapozaliwa na kutambua na kujitambua. pia, ndipo inaweza kutokea akajikuta huko.

Akasema kumbe kinachomfanya awe hivyo ni mazingira? Nikasema, ndiyo, kwani jamii ndiyo inayomtengeneza mtu awe hasi au chanya. Nikaona tunaelewana na tuko njia moja. Akahama huko.

Akaniambia hebu nikupe mfano huu, hivi mtu akiugua, nini anatakiwa kufanya? Nikamjibu, ni kwenda hospitali kutafuta matibabu. Akajibu, swadakta. Enhee! baada ya hapo je? Nikamjibu, akifika hospitali lazima aonane na daktari.

Naye akadakia kuwa lazima ahojiwe na daktari kuhusu kiini cha matatizo yake, na hasa mazingira aishimo pengine yamechangia ugonjwa na kisha apelekwe maabara kwa vipimo kujua hasa tatizo kitaalamu.

Nikamwacha atiririke bila kumkatiza. Daktari akishapata majibu ya maabara atajua tatizo na dawa ya kumpa na kama ugonjwa ni mkubwa atamlaza wodini kuendelea na matibabu, huku wauguzi wakimfuatilia na kutoa taarifa.

Hali yake ikishatengemaa, ataruhusiwa kutoka, na kupewa dawa za kutumia na ndugu zake kuchukua nafasi ya wauguzi, kumfuatilia anavyoendelea akiwa nyumbani ili ugonjwa usimrudie. Kisha akaniuliza kama nimeelewa.

Bila shaka alinishusha kiwango mpaka cha kati ya darasa la kwanza na la nne, kutokana na maswali hayo ambayo ni rahisi, lakini akilenga kunipa ujumbe ambao pengine katika makala yale sikuuweka.

Mimi nilipinga kitendo cha kuwaendekeza wafungwa mpaka kuwalipa posho, ili wakitoka wakaanzie maisha, nikisema hiyo itawafanya baadhi yao kutoka na kutaka warudi, jela kuendelea kulipwa posho. Lakini, jamaa yangu huyu hakuwa huko kabisa.

Baada ya mfano wa mgonjwa, akaniambia mchakato huo ndio pia unaopaswa kufuatwa kwa mfungwa kabla, wakati na baada ya kutoka jela. Ni Kwamba, anapoingia lazima historia na mazingira ya anakotoka vijulikane na kwanini yuko pale.

Akaniambia ni tofauti na ninavyofikiri, kwamba gerezani ni mahali pa adhabu, ni kwamba fikra hizo zilishaondoka miaka mingi na gerezani kubaki mahali pa kurekebisha tabia, hivyo ndiyo sababu ya kutaka mfungwa kabla ya kuanza kifungo ajulikane asili yake.

Akasema, gerezani ni mahali pa kurekebisha tabia, lakini kwa kujifunza stadi fulani fulani zitakazomsaidia, ili akitoka akafanye kitu uraiani. Hivyo, wizara zote lazima ziwe na sehemu ya mchango katika kumrekebisha mfungwa kwa kumpa mafunzo.

Akaniambia mfano mtu atokaye Ukerewe ukamweka gerezani, badala ya kumpa stadi ya uvuvi ukampa za ujenzi au useremala. Kwamba asili yake ya uvuvi, inahitaji mwendelezo wa kitaalamu zaidi. Nikajiuliza, je kama anatoka Ukuryani afunzwe nini, Uhayani je?

Lakini,akaniambia pia hizo posho zisemwazo si posho pesa, bali ni stadi na kama kuna mfungwa atafanya vizuri, basi apewe zawadi hata kama ni pesa na zipelekwe nyumbani kwake kusaidia familia, kwani kumfunga mtu na familia ikabaki bila ya msaada, ni kuzaa 'panya road' zaidi.

Kwa kifupi kutokana na muda, yeye alitaka pia mazingira ya nyumbani atokako mfungwa yajulikane kwa serikali, ili kifanyike kitu ili kwamba atokapo jela asiwe tena na ushawishi wa kutaka kurudi gerezani, kwa kuwa tu maisha uraiani ni magumu.

Nikamwuliza, je hiyo inawezekana hapa Bongo? Akanipa mfano kuwa Mkuu wa Magereza nchi fulani hivi Afrika, aliwahi kuwa mfungwa. Nilipotaka kudodosa ana maana gani, akaniambia, samahani sikujitambulisha kwako, mimi naitwa naniliu na

BIASHARA

# Shirika la Posta na ‘posta kiganjani’ kutoka zama sanduku posta pekee

**Mwandishi Wetu**




Huduma zikiendelea katika ofisi ya Posta, jijini Arusha. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

SHIRIKA la Posta Tanzania (TPC), ni la umma nchini na Afrika kwa ujumla, likiwa na historia ndefu kuanzia zama za barua kutawala katika sanduku la posta ,sasa likiendana na zama za mawasiliano kupatikana kidijitali.

Kwa siku za hivi karibuni, TPC imekuwa katika mabadiliko makubwa ya utendaji, muonekano wake umetawanyika nchi nzima, katika utendaji kazi zake ili zifanyike kidijitali na kukidhi matakwa na mahitaji ya jamii ya sasa.

Pia, liko katika maboresho ya miundo mbinu yake, kwa lengo la kwenda na wakati na kuwa shirika la kisasa. Postamasta Mkuu, Macrice Mbodo, anayataja maboresho hayo kuwa ni pamoja na kufanya ukarabati na uboreshaji majengo ya kutoa huduma za posta, mikoani na wilayani.

Kwa mujibu wa Postamasta Mkuu huyo, Shirika limeunda mifumo ya kiteknolojia kwa ajili ya kurahisisha utendaji na utoaji huduma kwa wananchi.

“Mfumo wa ‘Postal Management Information System (PMIS)’ umeundwa na kuunganishwa na huduma za barua, EMS, Posta kiganjani, ufuatiliaji yaani ‘track and trace’ na masanduku ya posta,” anasema na kuongeza kuwa:

“Mifumo mingine ni pamoja na kuimarisha mifumo ya kiuendeshaji ya kimataifa ya huduma za posta yaani CDS, IPS na IFS pamoja na kuanza matumizi ya ‘e-office’ kwa ajili ya kurahisisha utendaji na ufanyaji kazi za kiofisi” anasema.

Juma Chenge (45), ni mkazi wa Kijitonyama, Dar es Salaam anasema matumizi ya teknolojia yataliwezesha shirika kuwafikia watu wengi zaidi.

Kuhusu ulinzi wa mali za wateja, Mbodo anasema shirika limejiimarisha kwenye usalama na ulinzi wa mali zao, kwa kufunga mitambo mitatu kwenye Ofisi Kuu ya Dar es Salaam (GPO), katika maeneo muhimu ya ukaguzi wa vifurushi na kamera zaidi ya 330 kwenye ofisi zake za Bara na Visiwani.

Upande wa vitendea kazi, Chenge anasema, shirika limeongeza vitendea kazi kwa kununua magari 13 na pikipiki 20 zilizosambazwa kitaifa kwa ajili ya uendeshaji majukumu ya kufikisha bidhaa na huduma za kiposta waliko wateja.

“Pia, magari matano ya kusafirishia mizigo mizito yamenunuliwa na yanafanya kazi ya




Pa kutumbukiza barua.

kusafirisha mizigo mizito sehemu mbalimbali nchini” anasema na kufafanua, shirika limenunua huduma ya kidigitali ‘Posta Kiganjani’ inayompa mteja uwezo zaidi kupata huduma hizo.

Simu kiganjani na kupata huduma zote, inafungua na kumiliki Sanduku la Posta Mtandaoni (virtual box) na hivyo simu ya mteja ndiyo sanduku lake la barua,

“Sifa kuu ya sanduku la mtandaoni... ni kuwasiliana na mmiliki kwa njia ya SMS, hivyo inamfanya mteja wa huduma za posta asipate usumbufu wa kwenda mara kwa mara ofisi za posta kuangalia kama ana barua/kipeto/kifurushi,” anasema na kuendelea:

“Badala yake SMS hutumwa kwenye simu yake baada ya kitu chake kufika kwenye ofisi za posta na yeye kwa mapenzi yake kuchagua kuja ofisi za Posta kuchukua au kuagiza apelekewe pale alipo.”

Charles Masatu, mkazi wa Dar es Salaam na mtaalamu wa mawasiliano, anasema dunia kwa sasa imebadilika na ili kwenda na wakati, lazima taasisi au biashara ziwe za kidigitali.

“Uking’ang’ania mambo ya kizamani utabaki nyuma , nawapongeza Shirika la Posta kwa kujiongeza na hatua hiyo itawawezesha kuwafikia Watanzania wengi zaidi,” anasema

Postamasta Mkuu - Mbodo, anasisitiza ili kwenda na wakati na biashara za kimtandao, ndiyo mtazamo na mwelekeo wa biashara za posta duniani, shirika limeanzisha na kuimarisha maduka mawili ya kimtandao, ambako mteja huingia kwenye duka akitumia simu au kompyuta yake iliyounganishwa na intaneti.

“Huilipia kwa njia ya mtandao na husafirishwa kwa njia ya posta hadi mahali alipopachagua mwenyewe. Hadi sasa wajasiriamali takribani 810 wamesajiliwa kwenye duka la Posta mtandaoni ambalo kwa sasa yana wafanyabiashara waliosajiliwa.

Anasema, shirika limefanikiwa kuanzisha na kusimamia uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma mahala pamoja yaani “Huduma Pamoja Centres”na hadi sasa vituo vinne vimekamilika na kufunguliwa; Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya.

Postamasta Mkuu anafafanua, Shirika la Posta limeimarisha uhusiano kikazi katika uendeshaji na utendaji, kwa kuingia mikataba ya ushirikiano kibiashara, kiutendaji na uendeshaji taasisi 11 na wateja wakubwa 12 wa huduma za kiposta nchini.

Anasema kuna kuimarisha utendaji unaoendana na teknolojia za kidijitali na ndani ya mwaka huu mmoja hadi sasa, shirika limepokea wageni kutoka nchi za Ivory Coast, Kenya na Burundi, kujifunza uendeshaji huduma za posta wa kidijitali.

Katika utendaji, Postamasta Mkuu anasema TPC imeimarisha rasilimali watu yaani utendaji wa wafanyakazi ili kuongeza tija, akitoa mfano wa mafunzo na semina za kubaini viashiria hatarishi vya malengo, rushwa, anwani za makazi, itifaki, uadilifu, ubunifu na uongozi kazini, sambamba na mafunzo ya matumizi sahihi ya mifumo ya kisasa ya utendaji kiteknolojia.

**MIPANGO YA BAADAE**

Mbodo anasema, ili kujenga taswira chanya ya shirika TPC, malengo yaliyopo sasa ni kuhakikisha huduma zote na miradi iliyoanzishwa, inasambazwa kitaifa, ili kuhakikisha inawafikia Watanzania wote.

Mipango mingine anaitaja, ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu huduma za kiposta, ili kuhakikisha kila mwananchi anapata fursa ya kutumia huduma za Posta na kushirikiana na taasisi na mashirika mbalimbali.




Ujumbe uaohusu simu kiganjani.



# Nyumba 50 zavunjwa, wananchi wahaha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ZAIDI ya wakazi 50 wa eneo la Muhuji lililoko Mtaa wa Relini jijini Dodoma, wamekosa mahali pa kuishi baada ya nyumba zao kuvunjwa kwa madai kuwa eneo hilo ni la mwekezaji.

Katika tukio hilo, Jeshi la Polisi limelazimika kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya wananchi waliozuia gari lililobeba watumishi na mgambo wa jiji waliokwenda kubomoa nyumba hizo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Ufuatiliaji wa Mgogoro huo, Shabani Simba, ubomoaji huo umefanyika bila kushirikisha viongozi wa mtaa hali, ambayo inaibua hofu kwa wananchi.

Alisema eneo hilo bado lina kesi mahakamani na mahakama ilishatoa amri ya kusimamishwa kwa shughuli zote kwa pande zote mbili.

"Tunashangaa kuona leo hii wamekuja watu wa jiji pamoja na mgambo na polisi kusimamia ubomoaji wa nyumba zetu bila kutoa taarifa. Kibaya zaidi ni kwamba jambo hili bado liko mahakamani na kesi ni tarehe 24, mwezi huu na tulipewa maelekezo kuwa eneo hili lisiguswe na sisi wananchi au uongozi wa jiji. Tunashangaa wamekuja kutuvamia na kuanza kuvunja nyumba zetu," alisema Simba.

Pia alisema alisema kutokana na hali hiyo, wananchi waliamua kuunganisha nguvu na kuzuia gari, ambalo lilikuwa limebeba watumishi hao na mgambo wa kubomoa.

"Wananchi tumelazimika kutumia nguvu kulikamata na kuzuia gari lao ambalo walitaka kulitumia kukimbia baada ya kuona wananchi wamechachama wakiwa wamebea silaha mbalimbali za jadi," alisema.

Naye mkazi wa eneo hilo, Athumani Omary, alisema kitendo kinachokifanywa na jiji ni kukiuka sheria, miongozo na taratibu ambazo zilitolewa na mahakama kuhusu jambo hilo.

"Kutokana na kutokufuata taratibu kumesababisha familia hizi kukosa mahali pa kuishi baada ya makazi yao kuvunjwa wakati kesi, ikiwa bado inaendelea mahakamani," alisema.

Aloyce Mchenji, mkazi wa eneo hilo, alisema wananchi hawako tayari kuona haki yao inapotea na kumuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati mgogoro huo, ili wapate haki yao ya msingi.

"Tatizo linasababishwa na watu wa jiji ambao hawataki kuja kutupimia na kurasimisha makazi yetu wangetupimia hii hali isinge kuwepo," alisema.

Akizungumza na wakazi hao, Mkuu wa Kikuu cha Polisi Dodoma(OCS), Joram Samson, aliwataka wananchi kutojichukulia hatua mkononi bali wafuate sheria ili kupata haki yao.

"Naombeni hili gari mliachie kwani kulikamata ni kinyume cha sheria mimi nakitoka hapa nipele taarifa kwa Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Jiji, ili aje mjadiliane na muweze kupata suluhu ya jambo lenu,"alisema Samson.

Pamoja na OCS kuwaomba, wakazi hao hawakuwa tayari gari hilo kuondoka ndipo polisi walipoamua kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya.



Mkazi wa Mtaa wa Relini, eneo la Muhunji, kata ya Kizota, jijini Dodoma, akihamisha vyombo vyake baada ya nyumba yake kubomolewa na wanaodaiwa mgambo wa Jiji hilo juzi, kwa madai kuwa wamejenga kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya uwekezaji. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wataka upatikanaji vikaushio vya pareto

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI kwa kushirikiana na Bodi ya Pareto Tanzania imejipanga kuhakikisha vikaushio vya zao hilo vinapatikana kwa wingi, ili kuwa na pareto yenye ubora.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo, Lucas Ghadyo, akizungumza na Nipashe jana, alisema moja ya kero kubwa wanayokutana nayo wakulima wa zao hilo ni pamoja na sehemu ya kukaushia hali inayosababisha upotevu wa maua ya pareto.

"Bodi kwa kushirikiana na serikali tunaendelea na mchakato, ili kuhakikisha vikaushio vinapatikana tunahitaji kuona msimu huu wakulima hawapati changamoto ya sehemu ya kukaushia," alisema Ghadyo.

"Changamoto hii huchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza kiwango cha ubora cha Pareto kutokana na kutokauka vizuri," aliongeza.

Pia alisema wanatarajia kutoa elimu kwa wakulima katika maeneo mbalimbali, ili kuhakikisha wanaondokana na kilimo cha mazoea.

Alisema wanakwenda kufanya hivyo ili kuhakikisha wakulima wote wa zao hilo, wanapiga hatua moja mbele na kujiinua kiuchumi.

Alisema wamejiwekea mikakati ya bei elekezi ya pareto iliyopangwa, ili isaidie kumuwezesha mkulima kupata faida pindi anapoipeleka sokoni kuiuza.

Alisema bei elekezi ambayo imepangwa ni Sh.3, 200 kwa kilo ambayo wanaamini itamsaidia mkulima wa zao hilo kupata faida pale atakapoingia sokoni.

**Pia alisema wanatarajia kutoa elimu kwa wakulima katika maeneo mbalimbali, ili kuhakikisha wanaondokana na kilimo cha mazoea.**

# Waziri Aweso ataka Maji App kutumika

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameziagiza mamlaka na taasisi za maji kutumia mfumo wa simu ujulikanao 'Maji APP' kutoa takwimu sahihi za sekta hiyo ikiwamo utekelezaji wa miradi ya maji nchini.

Mfumo huo ulizinduliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan, ili sekta hiyo iwe na takwimu sahihi za maji na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya sekta hiyo.

Aweso alitoa agizo hilo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha maofisa maji wanaoshughulikia masuala ya takwimu na mifumo ya kielektroniki wa Maji APP.

Alisema mfumo huo utasaidia kutoa taarifa za maji kwa wakati na kwa usahihi, ili kujiepusha na malalamiko yanayojitokeza kwenye utoaji huduma za maji kwa wananchi.

"Wizara imekuwa na changamoto ya upatikanaji

wa takwimu kwa muda mrefu hivyo taasisi zote zinapaswa kuanza kutumia mfumo huu kama moja ya kutatua changamoto mbalimbali katika sekta ya maji. "Naomba taasisi zote zilizo chini ya wizara mtumie mfumo huo, kwa sababu utasaidia kupunguza malalamiko kwa wateja na kuongeza mapato na kupunguza upotevu katika sekta hii," alisema Aweso.

Alitoa onyo kwa maofisa hao kutopika takwimu na kutaka ziwasilishwe kwa menejimenti ya wizara kila mwanzo wa wiki.

"Viongozi wa wizara ya maji hakikisheni mnawawekea mazingira wezeshi maofisa takwimu hawa, ili waweze kufanya kazi ya uhakika na kutoa takwimu za ukweli badala ya kupika za uongo," alisema.

Hata hivyo, alisema hatasita kuwachukulia hatua kali kwa wanaokusanya takwimu na kuzikalia au kutoa takwimu za uongo.

Naye Mchumi wa Wizara, Lilian Nsimbo, akitoa maelezo ya mfumo huo, alisema pamoja na mambo mengine unawezesha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za maji na utekelezaji wa miradi ya maji inayoendelea kutekelezwa nchini.





# TRI kupambana na biashara haramu ya binadamu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI isiyokuwa ya kiserikali ya Tanzania Relief Initiative (TRI), inayojihusisha na masuala ya haki za binadamu imeanzisha mikakati ya kushirikiana na Wizara aya Mambo ya Ndani ya Nchi, kukabiliana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Taasisi hiyo kupitia mradi wake wa Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, imeanza kuwajengea uwezo watendaji wa vyombo vya usimamizi wa sheria ambavyo ni Jeshi la Polisi, Jeshi la Uhamiaji, mahakimu, waendesha mashtaka na maofisa ustawi wa jamii.

Akizungumza juzi jijini hapo wakati wa kutoa mafunzo kwa watendaji hao, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TRI, Laurean Rugambwa, alisema taasisi hiyo imeingia makubaliano maalumu na Kitengo cha Kuzuia Biashara ya Usafirishaji wa Binadamu cha Wizara ya Mambo ya Ndani (ATS).

Alisema mradi huo unalenga kuwajengea uwezo watekelezaji wa sheria pamoja na kupata maoni kutoka kwao ili kuandaa programu maalumu ambayo itasaidia kukomesha kabisa biashara hiyo nchini.

Alisema mafunzo hayo yanatolewa katika mikoa ambayo iko kwenye hatari zaidi ya kufanyika kwa biashara hiyo haramu na kabla ya kuanza Mbeya walishatoa kwenye mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Kagera.

Alisema mradi huo unafadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Ujerumani, Hanns Seidel Foundation (HSF), ambalo Makao Makuu yake yapo katika Jiji la Munich.

"Mkoa wa Mbeya upo kwenye huu mradi kwa sababu unapakana na nchi ya Malawi na pia uko jirani na mpaka na nchi jirani ya Zambia, pia Mbeya ni miongoni mwa mikoa yenye shughuli mbalimbali za uzalishaji ambazo zinachochea biashara ya usafirishaji wa binadamu ikiwamo kilimo, ufugaji na uchimbaji wa madini," alisema Rugambwa.

Aidha, alisema biashara ya usafirishaji wa binadamu ni miongoni mwa biashara kubwa zinazoisumbua dunia kwa sasa akieleza kuwa ni ya pili kwa ukubwa baada ya biashara ya dawa za kulevya.

Mwakilishi wa Sekretarieti ATS, Inspekta Selestine Makoba, alisema makundi yote yanayoshiriki kwenye mafunzo hayo ni yanayotekeleza Sheria Namba 6 na 8 za Mwaka 2008 za kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu nchini.

Alisema vita dhidi ya biashara hiyo ni ngumu na inahitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali katika kuikabili na mafunzo yanayotolewa kwa sasa yanalenga moja kati ya makundi muhimu kwenye vita hiyo.

Alisema kwa sasa biashara hiyo sio kubwa sana nchini kutokana na juhudi ambazo zimefanywa na serikali pamoja na wadau wengine kuanzia mwaka 2017 na alisema elimu imetolewa kwa kiwango kikubwa.

"Mafunzo haya tunaamini yatasaidia kuongeza uelewa kwa wadau hawa pamoja na wananchi wa kawaida maana pia mradi huu una eneo la kuwajengea uwezo viongozi wa ngazi za chini za serikali na kila mwaka ifikapo Julai 30, huwa yanafanyika maadhimisho ya kupinga biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu ambayo pia elimu hutolewa," alisema Inspekta Makoba.

Akifungua mafunzo hayo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ulrich Matei, alilishukuru Shirika hilo la TRI kwa kufadhili mafunzo hayo akisisitiza kuwa ni muhimu kwa ajili ya kukomesha biashara hiyo.

Alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni ya inayokabiliana na tatizo hilo la biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu kutokana na kuwa mpakani.

Alisema wahamiaji haramu wengi raia wa nchi za Ethiopia na Somalia, wanapitia katika mkoa huo kuelekea nchi jirani ya Malawi na wengi wao wamekuwa wakikamatwa pamoja na wenyeji wao.

"Hii biashara ni hatari sana, pale ofisini kwangu kuna magari mengi sana ambayo tumeyakamata kwenye biashara hii yakiwamo ya kifahari, sasa naamini kwamba mafunzo haya yanaenda kuwa suluhisho la kukabiliana na tatizo hili," alisema Kamanda Matei.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Tanzania Relief Initiative (TRI), Laurean Rugambwa, akizungumza na washiriki wa mafunzo ya siku tatu ya kuwajengea uwezo watekelezaji wa sheria ya kuzuia biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, yaliyoandaliwa kwa ushirikiano kati ya taasisi hiyo na Wizara ya Mambo ya Ndani, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## W'biashara wanaokwepa ushuru mazao waonywa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI wilayani Rungwe, imewatahadharisha baadhi ya wafanyabiashara wa mazao wilayani humo wanaokwepa kulipa ushuru na kodi zingine kuwa itawachukulia hatua kali za kisheria.

Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Vincent Anney, alitoa tahadhari hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazungumza na baadhi ya wafanyabiashara wa maparachichi wilayani humo kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu zao hilo.

Alisema baadhi yao wanakwepa kulipa tozo za kisheria na kusababisha halmashauri kukosa mapato na kushindwa kutekeleza baadhi ya miradi kwa ufasaha.

Aliwataka wakwepa kodi hao kuacha mara moja tabia hiyo ambayo ni kosa kwa mujibu wa sheria za nchi na endapo watapatikana wataanza kuwachukulia hatua za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine.

"Hatutaki kuanza kufukuzana na watu, lakini ikitubidi tutafanya hivyo, kuna baadhi wamekuwa wakikwepa kwa makusudi kulipa ushuru, tutaanza kumchukulia mmoja mmoja hatua za kisheria mpaka tukomeshe tabia hiyo," alisema Dk. Anney.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea kuwahimiza wananchi wa wilaya hiyo kulima kwa wingi maparachichi kwa kuwa ni miongoni mwa mazao yenye soko kubwa la ndani na nje ya nchi.

Aliwataka kuendelea kuzalisha kwa kutumia mbinu za kisasa ili kukidhi mahitaji ya soko la kimataifa pamoja na kuongeza uzalishaji kwa kutumia miche ya kisasa.

# Mbegu mpya maharagwe kukabiliana mabadiliko tabianchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini hapo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo, wamezalisha mbegu mpya za maharagwe ambazo zina uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, mbegu hizo zinadaiwa kuwa na uwezo wa kuzaa zaidi tofauti na za asili na kuwa na uwezo wa kuwainua wakulima kiuchumi na kuwahakikishia usalama wa chakula.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha wadau wa kilimo cha maharagwe kutoka katika mikoa minne ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini cha kutathmini mbegu mpya za maharagwe.

Dk. Bucheyeki alisema mbegu hizo zina uwezo wa kuhimili magonjwa na hali mbaya ya hewa ikiwamo mvua nyingi na hata ukame na kusisitiza kuwa uzalishaji wake hauna gharama kubwa ikilinganishwa na aina zingine.

Alisema mbegu hizo zinaandaa kufanyiwa majaribio katika wilaya 10 za mikoa minne ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kabla ya kuanza kusambazwa kwa wakulima wa mikoa mingine.

"Sasa hivi tunaenda kidigitali zaidi, hizi mbegu tunazifanyia tathmini kila mdau kwa njia anazojua yeye, lakini leo tunafanya ya pamoja ili tuwe na uhakika wa kile tunachowapelekea wakulima," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema kwa sasa kilimo kinahitaji kuwa na teknolojia za kisasa ili kiwe na tija kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa sasa yanaitesa dunia.

Mtafiti wa mbegu za jamii ya mikunde, Leonard Sabula, alisema wanakusudia kuyatumia maonyesho ya wakulima maarufu Nanenane kuzitangaza na kuzisambaza mbegu hizo kwa wakulima pamoja na kueneza teknolojia za uzalishaji.

Aliwataka wakulima wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuhudhuria maonyesho hayo kwa ajili ya kujifunza na kununua mbegu hizo ili wakazitumie kwa mwaka wa fedha ujao.

Alisema hivi karibuni walikuwa wanatekeleza mradi wa kupima afya ya udongo kwenye maeneo mbalimbali ya mikoa hiyo na watayatumia matokeo ya upimaji huo kuwashauri wakulima namna ya uzalishaji wa maharagwe na mazao mengine.

"Mbali na maharagwe haya pia tuna mbegu za soya ambazo tumezizalisha wenyewe hapa na ni mbegu ambazo zinazaa sana, wakulima wachangamke maana kwa sasa soko lipo la kutosha katika nchi ya Uchina," alisema Sabula.



# SMZ yasema imejipanga uchaguzi 2025

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema serikali imejipanga kufanikisha uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Aliyasema hayo ofisini kwake Vuga mjini Zanzibar wakati akizungumza na timu maalumu ya tathmini ya uchaguzi kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Hemed alisema kawaida serikali inajipanga kuendesha uchaguzi kila unapotokea nchini hasa uchaguzi mkuu, hivyo alitaka timu hiyo kusaidia kuwaongezea uwezo watendaji wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) na kutoa elimu kwa wananchi kujua umuhimu wa uchaguzi kwa lengo la kuimarisha amani, utulivu na kukuza demokrasia.

Alisema suala la elimu ni muhimu kwa sababu watu kadhaa huwa na uelewa mbaya hasa katika kipindi cha uchaguzi mkuu. Alisema baadhi ya watu wanafikiria kufanya mambo kinyume cha sheria za nchi na sheria za uchaguzi.

Makamu huyo alisema kuwa serikali inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Mwinyi tayari imeshayafanyia kazi kasoro zote zilizojitokeza kwenye uchaguzi uliopita na kuahidi kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa mtu au taasisi yoyote kwa maslahi ya Wazanzibari.

"Nitoe wito kwa wananchi wa kuwaeleza ukweli na uhalisia wote uliopo wageni mbalimbali waofika nchini kwa lengo la kujua hali ya kisiasaa kuimarisha ushirikiano na kudumisha amani na umoja kwa maslahi ya Wazanzibari wote kwa lengo la kukuza maendeleo nchini," alisema.

Kiongozi wa timu hiyo, Mwakilishi Mkazi wa UNDP Tanzania, Cristine Musisi, alisema watakahihisha wanatoa msaada wa hali yoyote kwa serikali utakapohitajika ili kuleta ufanisi wa kazi hasa kwenye uchaguzi.

Alisema UNDP kupitia mazungumzo hayo, itaendelea kusaidia na kutoa ushirikiano kwenye uchaguzi na maeneo mengine kwa maendeleo ya nchi.

# Rais Mwinyi ahimiza mafunzo lugha Kireno

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewashauri mabalozi wa Jumuiya ya Nchi Zinazozungumza Kireno (CPLP) kutoa fursa ya masomo ya juu katika nchi hizo kwa Wazanzibari.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu Zanzibar, alipokutana na mabalozi hao wakiongozwa na Balozi wa Angola nchini Tanzania, Sandro de Oliveira. Pamoja na mambo mengine, Rais Mwinyi na mabalozi hao walizungumzia haja ya kukuza matumizi ya lugha ya Kireno nchini.

Mabalozi wengine wa CPLP ni pamoja na Antonio Cesare wa Brazil, Konseli Mkuu wa Msumbuji Agostino Abakar Trinta na Mwakilishi wa heshima nchini Brazil Abduswamad Abdurahim.

Dk. Mwinyi alisema serikali inaunga mkono dhamira ya CPLP ya kutoa fursa kwa Wazanzibari kujifunza Kireno na kubainisha umuhimu wa kuanzia programu hiyo katika ngazi za vyuo vikuu.

Alisema ili kufanikisha dhamira hiyo, ni vyema mataifa hayo yakatoa fursa za masomo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini ili kujifunza lugha hiyo kikamilifu katika mwaka wa mwanzo wa masomo yao.

Utaratibu kama huo, alisema ndio unaotumiwa na mataifa mbalimbali duniani yakiwamo Uturuki; China na Russia ambapo wanafunzi kutoka nje ya nchi hujifunza lugha za mataifa hayo katika mwaka wa mwanzo wa masomo, kabla ya kuanza masomo ya fani husika.

Alisema Zanzibar kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) inayo taasisi inayohusika na masuala ya lugha, 'yaani Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni ambayo alisema ni kiungo muhimu katika kufanikisha dhamira hiyo.

Pia alisema kuwapo kwa filamu zilizoandaliwa kwa lugha ya Kireno na kuwekewa maelezo ya lugha ya Kiswahili au Kiingereza chini yake na hatimaye kuonyeshwa katika matamasha mbalimbali nchini kama vile Tamasha la Nchi za Jahazi (ZIFF) itasaidia kwa kiasi kikubwa kukuza matumizi ya lugha hiyo.

Nao mabalozi hao walimweleza Dk. Mwinyi dhamira yao ya kuendeleza ushirikiano na Zanzibar kupitia ukuzaji wa matumizi ya lugha ya Kireno.

Aidha, waliahidi kuendeleza ushirikiano na kufanya kazi pamoja na serikali ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Joseph Kilangi (katikati), akizungumza wakati akikagua miradi ya maji katika kisiwa cha Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mkataba ujenzi tangi maji hatihati kufutwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Joseph Kilangi, ameahidi kusitisha mkataba na kampuni ya Simba Developer inayojenga tangi la kuhifadhia maji safi na salama eneo la Mgeni Haji, Wilaya ya Magharibi A, Unguja.

Amesema kusudio hilo linatokana na serikali kutoridhishwa na utendaji kazi wa kampuni hiyo.

Kilango aliyasema hayo alipofanya ziara ya kiutendaji ya kukagua miradi ya maji inayotekelezwa na kampuni mbalimbali zikiwamo kampuni ya Afcom, Simba Developer na Shanjo.

Alisema utekelezaji wa kampuni hiyo haujafikia hata asilimia 30 ya kazi, hivyo endapo ujenzi huo utaendelea kudorora, atashauriana na mwasheria wa wizara ili kuandaa utaratibu wa kusitisha mkataba pamoja na kuitoza fidia kampuni hiyo.

"Mradi wa ujenzi la tangi ni mradi wa miezi minane lakini hadi sasa miezi minne imepita wamechimba shimo na kufunga nondo chini basi. Hakuna kazi inayoendelea, hivyo hatuwezi kuendelea na kampuni hiyo.

"Nitakaa na mwanasheria kuangalia namna ya kuvunja mkataba na kuwatoza faini wailipe serikali kwa sababu wameshatupoteza muda. Serikali haitaweza kufanya nao kazi tena," alisema Kilangi

Alisema hatua ya kukatisha mkataba itafanyika kwa kampuni zote ambazo zitashindwa kutimiza ahadi kama waliyokubaliana na kila kampuni ina muda kwa mujibu wa makubaliano katika kutekeleza mradi, hivyo hakuna kuongeza muda.

Mradi wa maji unatekelezwa na kampuni ya Afcon kupitia fedha za Benki ya Exim ambazo ni mkopo nafuu wa dola milioni 92.18. Mradi huo unahusisha kuchimba visima, kujenga matangi ya kuhifadhia maji, kufukia maboba na kujenga nyumba ya kuhifadhi maji (Maji House) na unaendelea vizuri,

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu huyo alitembeleza kisima cha maji katika Kijiji cha Bumbwisudi na kuonyesha kuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo na nakusema kitapoanza kutumika tatizo la maji litakuwa historia kwa mji wa Zanzibar.

Alisema kisima hicho kina uwezo wa kusukuma maji lita 250,000 kwa saa moja kwa mujibu wa wataalam na maji hayo yatapelekwa katika tangi la Welezo na kusambaza katika wilaya ya Mjini Unguja.

Kilangi pia alitembelea mradi wa maji unaotekelezwa na kampuni ya Shanjo kupitia fedha za ahueni za UVIKO-19 katika Shehia ya Mbuzini Wilaya Magharibi 'A" wenye thamani ya dola bilionii 34.2. alielezea kuridhishwa ma utekelezaji huku akiwasisitiza wataalam kuongeza kasi ya utendaji.

Naye Meneja Mradi, Rashid Mohamed kutoka Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), alisema mradi wa kisima kupitia fedha za ahueni za UVIKO-19 unatarajia kujenga matangi 10 kwa Unguja na Pemba, kuchimba visima vipya 38 na kufanya kazi ya kutandika mabomba.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**OMBI LA URAIA**
**LA JANICE ITUMBI KILONZO**



Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, utaifa wake kwa sasa ni **MKENYA** nchi atokayo **KENYA** shughuli zake ni **MAMA WA NYUMBANI** anwani yake ni **S.L.P 6090 DSM.**

Yupo hapa nchini tangu mwaka 2004. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, S.L.P 512 Dar es salaam. KUMB. NA. DN 468659.

..........................................................................
**Kny: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI TIN NUMBER

**SALIM HAMIS MHANDO** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 902 DLC – ISUZU FIGHTER. TIN** number ya **TRA 109-643-653. Y**eyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa za polisi:
**DAR/JNI/RB/260183/2022 na DAR/JNI/RB/260176/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EDWARD ELIAS MAKWI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4453/0058** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHULE YA SEKONDARI MACHIMBONI** mwaka **2019** . kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: KAT/MPA/RB/252781/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**THOMASI JOHANSEN BYARUGABA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0155-0650** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **TABORA BOYS SECONDARY SCHOOL** mwaka **2016**. kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/GOG/RB/502158/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**OTHMAN SWABRI MSUYA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index namba **S2376-0147** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MUGABE SEKONDARI** mwaka **2011.** Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **TAARIFA YA POLISI: DSM/PHQ/RB/279564/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI BAJAJI

**GODLOVE SHIWARYAELI MUNISI** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba MC866CBM, CHASSIS NAMBA:**MD6M14PA9J4K65605**, ENGINE NAMBA: **AK4K14478201**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/OST/RB/330659/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOFREY ZACHARIA MUHOZYA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ZAKIA MEGHJI SECONDARY SCHOOL** mwaka **2017.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: WMB/RB/432/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**DAVID PRAISE OMONDI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0631-0080** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **UMOJA** Sekondari mwaka **2016.** Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S5244-0507** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **WAJA BOY'S SEKONDARI** mwaka 2019. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: DSM/PHQ/RB/278799/2022.**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**
**BILL OF COST NO.7 OF 2020**
**EDWARD HELGARD SAM ......DECREE HOLDER**
**VERSUS**
**PRIDE TANZANIA GRM AUCTIONEER & COURT BROKER.....JUDGEMENT DEBTOR ROBERT KIMARO**
**TO:**
**GRM AUCTIONEER & COURT BROKER ,**
**WHEREVER YOU ARE.**

**NOTICE FOR MENTATION**

**TAKE NOTICE :** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 22nd September,2020 at 09:00 am before Honourable
**O.H. KINGWELE** -Deputy Registrar.
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this **14th day of August ,2020**

O.H.KINGELE
DEPUTY REGISTRAR
**O.H.KINGELE**
**DEPUTY REGISTRAR**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KANDA YA BUKOBA**
**MAOMBI NA84/ 2021 YANAYOTOKANA NA RUFAA YA MADAI Na. 151/2018**
**GRACE MAHUMBUKA ..............MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**FRANK MUGANYIZI..........MJIBU MAOMBI**

**WITO/ KUITWA SHAURINI**

**Kwa FRANK MUGANYIZI**
**Popote ulipo**
Hii ni kukutaarifu kwamba shauri la rufaa tajwa juu imepangwa kusikilizwa tarehe 27 mwezi Julai mwaka 2022 saa 3:00 asubuhi, mbele ya Mh. Jaji A. E. MWIPOPO wa Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba. Kwa hiyo unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria. Endapo hutohudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako shauri hili litasikilizwa bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 22 mwezi Juni mwaka 2022.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**BUKOBA.**

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**NDUGU NGASA MUSSA KULWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Trekta yenye jina la **ANNA ODIRO MTITU** na namba za usajili **T452 AZY** aina ya **MASSEY 375** Rangi Nyekundu yenye Chasis **No. 7001701,** Engine **No.502450P.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba
**DOD/DOD/RB/277893/2022**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
Probate and Administration Cause No.97 of 2022
In the matter of the estate of the late of the late
**VICENT FIDELIS CHALLE**
**AND**
In the matter of application for letters of administration by
- **REGINA CHALLE BARANKENA**
- **PUDENSIANA CHALLE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 of 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **12 Day of AUGUST, 2022**
**Dated at Dodoma this 13 day of July,2022**

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRIC
**RESIDENT MAGISTRATE**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT SONGEA**
**APPELLANT JURISDICTION**
**PC/MISC/CR/REV/APPLICATION NO. 2 OF 2022**
**(from original case No. 7 of 2021**
**In the district court of NAMTUMBO at NAMTUMBO-RUVUMA**
**ZIANABU ZUBERI LUSINGA ...........APPELLANT**
**Original/accused**
**VERSUS**
**AYUBU SAID MAKALE.................RESPONDENT**
**Original prosecutor**

**TO AYUBU SAID MAKALE**
**P.O.BOX, NAMTUMBO**

**NOTICE OF DATE HEARING/ MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been set fixed for hearing of the appeal against conviction and sentence filed by the APPELLANT
You are required too appeal in this court on the 21 Day of 7 2022 at 14:00 PM or soon thereafter, Before **Hon U.E NADEHA JUDGE**
**GIVEN UNDER** my hand and the seal of the court, this **13 day 7 2022**

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI BAJAJI

**ATHUMANI SALUM**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI AINA YA PIAGGIO YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 723 BUU . KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
**TAARIFA YA POLISI**
**KAH /RB/ 479/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOEL DONALD MASHIMBA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SANLG YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 771 CKL.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
**TAARIFA YA POLISI**
**KAH /RB/ 293/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**JACKSON JUSTINE ELIA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI AINA YA PIAGGIO YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 771BSK .**
KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISITAARIFA YA POLISI
**KAH /RB/ 479/2022**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF GEITA**
**AT GEITA**
**MISC. CIVIL APPLICATION No. 14 OF 2022**
**WERONS MICRO CREDIT LIMITED........................APPEALANT**
**VERSUS**
**DANIEL HAJI MAYUYA ....RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE FOR MENTION**
**TAKE NOTICE THAT,** the aove case has been fixed for mention on the 18th day of July, 2022 at 09.00 am
**YOU ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case
**GIVEN UNDER MY HAND** and the **SEAL** of the court this **28th day of june 2022**.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
GEITA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA.08/2022**
**(Asilia shauri la Ardhi Na.28/2021 kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Mbeya,asilia shauri la ardhi Na.18/2020 kutoka Baraza la Kata ya Ihahi)**
**LAZARO MTAMAGILA............MRUFANI**
**DHIDI YA**
**UPENDO MWALUGAMBA...............MJIBU RUFAA**
**KWA BIBI:UPENDO MWALUGAMBA**
**POPOTE ULIPO-TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**
Unaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 23/08/2022 siku ya Jumanne,saa 3:00 asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA,ukikosa kufika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama leo hii tarehe 23/06/2022.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

## NGOMENI ENTERPRISES

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA NA NOTISI YA KULIPA DENI.**

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na crdb bank makao makuu Dar es salaam tunatoa notisi ya siku nne (14) tu ili uweze kulipa deni lako lote unalodaiwa. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA / MAHALI | TAREHE/ MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | MAIUM ELISANTE DAFFA | KIHONDA AZIMIO | 3.8.2022 SAA 2 ASUBUHI |
| 2. | YUSUPH ABDALLAH | LUKOONI - CHANIKA | 29.7.2022 SAA 3 ASUBUHI |
| 3. | SALEHE MOHAMED ALLY | KIBONDE MAJI "A" CHARAMBE | 2.8.2022 SAA 3 ASUBUHI |

**MASHARTI YAMNADA.**
1. Dhamana itauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya asilimia 25 ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na asilimia 75 atalipa ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la asilimia 75 katika muda uliopangwa hapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyuma na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**MAWASILIANO:**
**CRDB BANK PLC, HEAD QUARTER.**
**NGOMENI ENTERPRISES, DSM. SIMU: 0719974916/ 0784252048**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Russia, Ukraine ni piga nikupige

**KYIV,** UKRAINE

MAPAMBANO makali kati ya Russia na Ukraine yanazidi kurindima, huku makombora yakirushwa kila upande na kusababisha hali kuwa mbaya mashariki mwa Ukraine.

Hata hivyo, Russia imekanusha kuwa na mpango wa kununua ndege zisizo na rubani kutoka Iran ili kuendelea na mpango wake wa kuteka miji mbalimbali katika eneo la Donbas.

Msemaji wa rais wa Russia, Dymtry Peskov,alisema Rais Vladimir Putin, hana mpango wa kujadili uwezekano wa kununua ndege zisizo na rubani kutoka Iran katika ziara yake atakayoifanya nchini humo.

Peskov alisema iwapo kuna mpango wowote wa kununua vifaa kama hivyo kama ilivyodai Marekani ingefahamika. Mshauri wa usalama wa kitaifa wa Marekani Jake Sullivan, alisema Marekani ina taarifa kwamba serikali ya Iran inajiandaa kuipa Russia mamia ya ndege zisizo na rubani zikiwemo zinazoweza kubeba silaha.

Iran imekanusha taarifa hiyo ya Marekani ikisema, ni kweli kuna ushirikiano kati yake na Russia, lakini ulianza hata kabla ya vita vya Ukraine.

Ikulu ya Kremlin ilitangaza juzi kwamba Putin atasafiri kuelekea Iran kukutana na Rais Ebrahim Raisi na Rais Reccep Tayyip Erdogan wa Uturuki

### RUSSIA YARUSHA MAKOMBORA

Makombora tisa kutoka katika mfumo wa makombora ya kupambana na ndege ya S-300, yalirushwa kwenye kituo kilichopo eneo la Mykolaiv.

Kulingana na ripoti ya OVA, makombora hayo yamesababisha uharibifu katika taasisi mbili za elimu, kituo cha miundombinu na hoteli.

Meya wa Mykolaiv, Oleksandr Sienkovych, alifafanua kuwa hoteli iliyoko katikati mwa jiji imeharibiwa.

Kituo cha ununuzi na burudani kilichopo mkabala na hoteli hiyo nacho kiliteketezwa na kubaki kifusi.

Wakati huo huo, watu wanne walifariki na wengine wawili walijeruhiwa baada ya kushambuliwa kwa kijiji cha Novoselivka katika eneo la Pervomaysk.

### RUSSIA YADAIWA KUSAJILI KURUTI

Russia inadaiwa iliamuru kusajili watu wakujitolea kupigana katika vita, badala ya kutangaza uhamasishaji katika baadhi ya sehemu.

Wataalam katika Taasisi ya Marekani ya Utafiti wa Vita (ISW), waliandika katika ripoti nyingine kwamba kuna dalili ya kuwepo na usajili wa askari hao hivi karibuni.

Mwandishi wa habari wa masuala ya kivita na mwanablogu, Maxim Fomin alisema kuwa 'uhamasishaji wa hiari umeanza nchini Russia, ambapo kila eneo lazima liunde angalau kikosi kimoja cha kujitolea.

Inadaiwa Kremlin iliamuru maeneo 85 ya serikali, ikiwamo Sevastopol iliyotekwa na Crimea, kusajili na kuwahamasisha kifedha watu wa kujitolea kuunda vikosi vipya.

Kulingana na ripoti za vyombo vya habari vya Russia, mamlaka za kikanda huajiri wanaume walio na umri wa chini ya miaka 50 au 60 kwa taaluma fulani za kijeshi kwa mkataba wa miezi sita na kutoa wastani wa mshahara wa rubles 220,000 hadi 350,000 kwa mwezi sawa na dola 3,750 na 6,000.

Wataalamu wa ISW wamehesabu kwamba ikiwa kila eneo litaunda angalau kitengo kimoja cha kijeshi cha watu 400, jumla ya idadi ya wanajeshi wa kujitolea inaweza kufikia watu 34,000.

### HATUA YA KWANZA YAFIKIWA

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, amesema hatua muhimu ya kwanza imefikiwa katika juhudi za kuwezesha nafaka kusafirishwa kutoka Ukraine.

Guterres alieleza kwamba hatua hiyo imefikiwa kwenye mazungumzo ya mjini Istanbul kati ya wajumbe wa Russia na Ukraine.

Katika mkutano huo wajumbe wa Umoja wa Mataifa na Uturuki pia walishiriki.

Guterres alielezea matumaini ya kupatikana makubaliano rasmi wiki ijayo.

Alisema kwa jumla pana makubaliano juu ya mpango wa Umoja wa Mataifa wa kusafirisha mamilioni ya tani za nafaka kutoka Ukraine na kufikisha kwenye masoko ya kimataifa na pia kuiwezesha Russia kuuza nje nafaka na mbolea. Vikwazo vya kimataifa dhidi ya Russia vimeongeza bei ya mbolea, ambayo inasababisha kupanda kwa bei ya chakula.

Naye Waziri wa Ulinzi wa Uturuki, Hulusi Akar aliyeshiriki kwenye mazungumzo hayo amefahamisha kuwa pande zote zimekubaliana juu ya udhibiti wa pamoja kwenye bandari na kwenye njia nyingine ili kuhakikisha usafirishaji salama. Mpango huo uliopendekezwa na Umoja wa Mataifa utawezesha kusafirishwa shehena hizo za nafaka kupitia njia maalum, zitakazoepuka maeneo ya hatari.

### UKRAINE YAHANGAIKA KUSAFIRISHA NGANO

Takriban tani milioni 22 za nafaka zimezuiliwa nchini Ukraine, na shinikizo liliongezeka kila siku la kutafuta suluhu ambayo ingewezesha kusafirisha ngano kutoka kwenye maghala yake.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo FAO, limesema vita vya nchini Ukraine vinahatarisha juhudi za usambazaji wa chakula kuelekea kwenye mataifa mengi yanayoendelea, na hivyo kusababisha kuongezeka kwa bei ya chakula duniani kote. **BBC**

# Jasusi wa Gambia ahukumiwa kifo

**BANJUL,** GAMBIA

JAJI mmoja nchini Gambia amemhukumu kifo aliyekuwa mkuu wa upelelezi wa nchi hiyo, Yankuba Badjie, na maofisa wengine wanne wa usalama kwa mauaji ya mwaka 2016.

Mauaji hayo yalifanywa kwa mwanaharakati wa kisiasa katika siku za mwisho za utawala wa kikatili chini ya Rais wa zamani Yahya Jammeh.

Mwanaharakati huyo, Ebrima Solo Sandeng, kiongozi mkuu katika chama cha upinzani cha United Democratic Party, alikuwa amekamatwa wakati wa maandamano ya kuipinga serikali.

Alikufa gerezani siku mbili baadaye, baada ya kupigwa na kuteswa.

Kifo chake kilichochea wimbi la hasira ya wananchi ambayo hatimaye ilisababisha kuondolewa madarakani kwa Rais Jammeh baada ya miaka 22 madarakani.

Jammeh alikimbia mwaka wa 2017 hadi Equatorial Guinea, ambako bado yuko uhamishoni. **DW**



Waandamanaji wakiwa wamekaa katika chumba cha mkutano ndani ya ofisi ya Waziri Mkuu wa Sri Lanka mjini Colombo jana, baada ya kulikalia jengo la kiongozi huyo kwa siku kadhaa wakishinikiza ajiuzulu. **PICHA: AFP**

# Biden awasili Mashariki ya Kati

**TEL AVIV,** ISRAEL

RAIS wa Marekani Joe Biden, ameanza ziara yake ya kwanza ya Mashariki ya Kati jana, katika mkakati wake wa kuimarisha ushirikiano na nchi za ukanda huo.

Biden alipowasili nchini Israel, alisema Marekani na Israel zina uhusiano imara wa ndani.

Aliahidi kuimarisha zaidi uhusiano wa kiuchumi kati ya nchi hizo mbili katika siku zijazo.

"Tutauendeleza utangamano wa Israel katika eneo hili, tutapanua mawasiliano kama ule mkutano wa kilele wa I2U2 ambao utazileta pamoja Israel, Marekani, Umoja wa Falme za Kiarabu na India ili kuongeza ushirikiano wa kiuchumi kati ya Mashariki ya Kati na Indo-Pasifiki. "alisema kiongozi huyo.

Rais huyo wa Marekani hakutaja mojawapo ya malengo makubwa ya ziara yake akiwahakikishia maofisa wenye wasiwasi wa Israel na Saudi Arabia kwamba amedhamiria kuizuia Iran kuwa nguvu ya nyuklia.

Maofisa wa Israel walisema mpango wa nyuklia wa Iran unaokuwa kwa haraka uko juu kwenye ajenda ya mazungumzo na rais huyo wa Marekani. Kuufufua mkataba wa nyuklia wa mwaka 2015 na Iran ndicho kilichokuwa kipaumbele cha Biden alipochukua madaraka.

**DW**

HABARI MICHEZO

# ASUKILE AFUNGUKA PRISONS WAMENUSURIKA AIBU BARA

**Na adam Fungamwango**

NAHODHA wa Prisons, Benjamin Asukile ambaye alifunga bao la kusawazisha katika mechi ya marudiano ya 'play off' dhidi ya JKT Tanzania, ameeleza kufurahishwa na timu yake kubaki kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara huku akisema ingekuwa ni aibu kubwa kama timu hiyo ingeshuka daraja.

Katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Asukile alifunga bao lililoinusuru Prisons na janga hilo la kuteremka na kufanya matokeo ya jumla kuwa mbele kwa mabao 2-1.

Prisons ilipata ushindi wa bao 1-0 katika mechi ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo ulioko Mbweni jijini Dar es Salaam.

"Niliwaambia watu, nikawaambia mashabiki, na wachezaji wenzangu tufanye njia yoyote ile ili timu ibaki Ligi Kuu. Ingekuwa aibu sana kwa timu kubwa kama Prisons kushuka daraja kutokana na jinsi viongozi wa Magereza wanavyotupa sapoti, wapo karibu na timu na kuihudumia, wengine ni askari Magereza wote Tanzania nzima wanatupa sapoti, pia ina mashabiki wengi hapa Mbeya, kwa hiyo isingekuwa vizuri.

Baada ya kutanguliwa bao kama mzoefu nikatafakari la kufanya nikaona hapa ni lazima nifanye kitu kwa sababu tungekwenda kwenye penalti lolote lingeweza kutokea, kwa bahati nzuri nikafunga bao," alisema mchezaji huyo wa siku nyingi kwenye timu hiyo.

Aliongeza baada ya kufanikiwa kubakia kwenye ligi hiyo, watajipanga vyema ili kutorudia makosa hayo tena na kuwaahidi mashabiki wa Prisons sasa wajiande kupata furaha.

Kocha Mkuu wa Prisons, Patrick Odhiambo alisema mechi ilikuwa ngumu kwa sababu kwanza ilikuwa ni 'dabi' ya maafande, lakini pia ilikuwa ni mechi ya kusaka matokeo tu.

"Ilikuwa ni lazima timu ishinde, hivyo zilijikakamua. Tumefanikiwa kubaki ni lazima sasa tufanye usajili kwenye nafasi zenye udhaifu ili yasijirudie tena haya," alisema Mkenya huyo.

Naye Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Mohamed Abdallah 'Bares' alisema mpira umeisha, haikuwa bahati yao, lakini akawasifu wachezaji wake kwa kupambana.

"Wenzetu wamebebwa sana na bao la nyumbani kwetu, ndiyo lililotutoa, lakini vijana wangu wamepambana, ligi imeisha tunaenda kujipanga upya na Ligi ya Championship," Bares aliongeza.

Biashara United na Mbeya Kwanza ndio timu nyingine zilizoshuka daraja moja kwa moja na msimu ujao zitashiriki Ligi ya Championship huku Ihefu SC na DTB sasa Singida Big Stars.



Mchezaji wa timu ya soka ya vijana wa umri chini ya miaka 20 ya Azam FC (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya yosso mwenzake wa Polisi Tanzania katika mechi ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya U-20 iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex juzi usiku. Azam ilisonga mbele kwa ushindi wa penalti 6-5. **PICHA: TFF**

# Polisi Tanzania wamlilia Metacha

**Na Saada Akida**

WAKATI Polisi Tanzania wakisema kipa, Metacha Mnacha ni mchezaji wao halali, mabosi wa Singida Big Stars wamewataka kwenda kukaa meza moja ili kumaliza utata wa usajili wa mchezaji huyo wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), imefahamika.

Polisi Tanzania kupitia Msemaji wake, Hassan Kayozi imesema hawana sababu ya kukutana na Singida Big Stars kwa sababu wanatambua Metacha bado ana mkataba wa mwaka mmoja na timu yao.

"Tatizo liko kwa mchezaji husika kwa sababu anatambua bado ana mkataba na Polisi iweje asaini timu nyingine, alichokifanya ni kinyume na utaratibu na sheria za usajili kutoka klabu anayotumikia," alisema Hassan.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Singida Big Stars, Muhibu Kanu, aliliambia gazeti hili wao wamefuata taratibu zote katika kumsajili Metacha ambaye walimtambulisha rasmi hapo juzi.

Kanu alisema wao wamefuata taratibu zote za usajili kwa ajili ya kupata huduma ya kipa huyo kwa lengo la kuboresha kikosi cha timu yao.

"Hatuwezi kuvunja kanuni na sheria za soka kwa sababu tumejiridhisha juu ya Metacha na kumpa mkataba wa kuitumikia timu yetu kwa msimu mpya wa 2022/23," alisema Kanu.

## Ndayiragije, Geita Gold wamalizana

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Geita Gold imemalizana na aliyekuwa kocha wake mkuu, Ettiene Ndayiragije na hivyo kumaliza adhabu iliyopewa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA) la kufanya usajili.

Taarifa iliyotolewa na Mtendaji Mkuu wa Geita Gold FC, Simon Shija, imesema tayari klabu hiyo imeshatekeleza yote waliyoagizwa na sasa wapo huru kuendelea na mipango yake kama kawaida.

"Uongozi wa klabu ya soka ya Geita Gold unapenda kuwataarifu mashabiki, wadau na wapenda michezo imemalizana na adhabu ya FIFA iliyokuwa na zuio la kuifungia kufanya usajili.

Klabu umetekeleza matakwa ya kisheria na kikanuni kwa kuzingatia miongozo ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA) na sasa ipo huru kuendelea na utendaji wake. Tunaomba wadau kuendelea kushirikiana na klabu." Ilimaliza taarifa hiyo.

Ndayiragije alitimuliwa na mabosi wa timu hiyo tangu Oktoba mwaka jana akiwa ameongoza katika michezo minne tu.

## Mandonga ajipanga kumchapa Kaoneka

**Na Saada Akida**

BONDIA mwenye mikwara mingi nje ya ulingo, Karim Mandonga ameanza rasmi mazoezi ya gym kwa ajili ya kujiwinda kuelekea pambano lake dhidi ya Shabani Kaonekana litakalofanyika kwenye Usiku wa Deni (PAYBACK NIGHT) Julai 30, mwaka huu mjini Songea mkoani Ruvuma.

Mandonga aliliambia gazeti hili ameamua mbali na kufanya mazoezi ya gym, ameandaliwa programu nyingine ili kuhakikisha anafuta makosa aliyoyafanya katika pambano lililopita.

Alisema amemtaka mpinzani wake ambaye naye anatamba kufanya vyema, ajiandae kupokea kipigo kwa sababu anataka kurejesha heshima baada ya kupoteza katika pambano lililofanyika Morogoro.

"Nimejiandaa vizuri zaidi kwa ajili ya pambano langu, Kaoneka ajipange, asije kichwa kichwa akadhani Mandoga ambaye alipoteza Morogoro atakuja kumpata katika pambano hilo la Ruvuma, nitakuja kivingine," alitamba Mandonga.

Kocha wa Mandonga, Said Said alisema ujio mpya wa bondia wake utaushangaza ulimwengu kwa burudani ya aina yake atakayoionesha katika pambano hilo.

Pambano kubwa siku hiyo litakuwa ni kati ya Mtanzania, Selemani Kidunda dhidi ya Eric Katompa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RONALDO ATAKIWA ARABUNI**
MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, amepata ofa yenye thamani ya euro milioni 300 ili kucheza misimu miwili kwenye klabu moja ya Saudi Arabia. ***(TVI and CNN Portuguesa, via AS)***

**MARTINEZ AKARIBIA UNITED**
MANCHESTER United wako katika hatua ya mwisho ya mazungumzo ya kumsajili, Lisandro Martinez kutoka Ajax baada ya kukubaliana maslahi binafsi na mlinzi huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 24. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

**AJAX YAZIDIWA NGUVU**
KLABU ya Ajax imekubali kushindwa kumzuia Lisandro Martinez asiondoke msimu huu, lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu Uholanzi wanataka ada ya pauni milioni 46. ***(Times)***

**KIMPEMBE ANUKIA PSG**
CHELSEA sasa inamwania mlinzi wa Paris St-Germain, Presnel Kimpembe mwenye umri wa miaka 26, baada ya kukubaliana ada na Napoli kwa ajili ya mlinzi wa kati Msenegali, Kalidou Koulibaly (31). ***(Guardian)***

**EVERTON YAMTAKA TRAORE**
KLABU ya Everton imeiambia Wolves itakubali kutoa ada ya pauni milioni 10 kwa ajili ya kumnasa winga wa Timu ya Taifa ya Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 26, msimu huu. ***(Football Insider)***

**LINGARD AGEUKA LULU**
KLABU ya mpya ya kocha, Wayne Rooney, DC United imeungana na timu zingine za Ligi Kuu Marekani (MLS) na Ligi Kuu England zinazomtaka nyota wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29, ambaye ametimka Manchester United. ***(Marca)***

**DE LIGT AJIONGEZA**
MLINZI wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 22, yuko tayari kupunguza mshahara wake ili kujiunga na Bayern Munich kutoka Juventus. ***(Bild)***

**LEWANDOWSKI AKARIBIA**
BARCELONA wako tayari kuongeza ofa yao kwa ajili ya mshambuliaji wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, hadi kufikia pauni milioni 42.3. ***(Bild)***

**LEEDS YAMTAKA MATA**
LEEDS United wanamtaka kiungo, Juan Mata mwenye umri wa miaka 34, ambaye yuko huru baada ya kuondoka Manchester United mwishoni mwa msimu huu. ***(AS)***

**CHELSEA, MOUNT KUTETA**
KIUNGO wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 23 anataka kuanza mazungumzo na klabu hiyo kwa ajili ya mkataba mpya wa muda mrefu. ***(Athletic)***

**DEMBELE MAMBO SAFI**
WINGA wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 25, atasaini mkataba mpya wa miaka miwili kusalia Barcelona baada ya mkataba wake wa awali kumalizika. ***(Sport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA AWEKA WAZI ALIPOKWAMA UNITED

Ataja mabadiliko ya makocha mara kwa mara na hali ya majeruhi ni...

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa Paul Pogba amesema "kila kitu" ikiwamo suala la "kocha, timu, nafasi" kilimzuia katika klabu yake ya zamani ya Manchester United.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 amejiunga tena na Juventus baada ya kuondoka United kufuatia mkataba wake na klabu hiyo ya Old Trafford kumalizika.

"Nafurahia mabadiliko niliyofanya katika maisha yangu", amesema Pogba akinukuliwa na BBC Sport.

"Mara nyingine unafanya chaguo ambalo halikufurahishi, lakini nafurahia miaka yangu pale Manchester, kwa sababu nilijifunza kuwa mwanaume."

Pogba ambaye alianza soka kupitia akademi ya Manchester United lakini aliondoka katika klabu hiyo mwaka 2012 na kujiunga na Juventus ambapo alishinda mataji manne ya Serie A na baadaye kuondoka na kurejea tena United kwa dau lililovunja rekodi ya dunia la pauni milioni 89 katika uhamisho wa mwaka 2016.

Alishinda Kombe la EFL na la Ligi ya Europa akiichezea United katika msimu wake wa kwanza akiwa na klabu hiyo, lakini yalikuwa mataji pekee aliyoshinda katika kipindi chake cha pili akiwa nao.

Alicheza chini ya Kocha Jose Mourinho, Ole Gunnar Solskjaer, Michael Carrick na Ralf Rangnick baada ya kurejea United na akashindwa kuonyesha kiwango chake bora kwa misingi thabiti chini ya kila mmoja wao.

Hata hivyo, Pogba, ambaye ana mechi 91 za kimataifa, alikuwa na ushawishi wakati Ufaransa iliposhinda Kombe la Dunia nchini Urusi mwaka 2018.

"Kubadilishwa kwa makocha (wa Manchester United) kila mwaka ni ngumu - hiki kilikuwa kipengele kigumu kwangu," alisema Pogba.

"Kisha kulikuwa na jambo la majeruhi, lakini nadhani pia lilikuwa jambo la kiakili kucheza na kutocheza kunakufanya upoteze kasi.

"Kwa kila kitu: kocha, timu na nafasi, haya yote yalinizuia.

"Sasa, hata hivyo, nimeondoka na utamwona Paul mwingine. Ninaweza kufanya vizuri zaidi kuliko miaka ya hivi karibuni."

Pogba amesaini mkataba wa miaka minne na Juventus, ambayo ilimaliza katika nafasi ya nne kwenye Serie A msimu uliopita.

Aliongeza: "Nimefurahi kurudi nyumbani, hivi ndivyo ninavyojisikia hapa. Hiki ni kitu zaidi ya ndoto. Nina furaha sana.

"Kulikuwa na timu nyingine zilizokuwa na nia, lakini moyo wangu ulichagua Juventus. Nilikuwa vizuri hapa awali na niko sawa sasa, nataka tu kufanya vizuri."

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,014,8

MECHI KALI

MELBOURNE VICTORY

VERSUS

MANCHESTER UTD

1 | 5.00

X | 4.26

2 | 1.50

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#,

CHAGUA 4

- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:

18+ 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# STERLING RASMI MALI YA CHELSEA



**LONDON, England**

CHELSEA wamekamilisha usajili wa winga wa kimataifa wa England, Raheem Sterling kwa mkataba wa miaka mitano kutoka Manchester City.

Klabu hiyo ya London ilikubali ada ya takribani pauni milioni 50 na wapinzani wao wa Ligi Kuu England na Sterling sasa ameondoka kwenye Uwanja wa Etihad baada ya miaka saba ya kuishi Manchester City.

Baada ya kufuzu vipimo vya afya jijini London, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 alisafiri hadi Florida kujiunga na ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani, Jumanne kabla ya kutambulishwa kama mchezaji wa Chelsea.

Sterling alikuwa ameingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na City na alionyesha nia ya kupata changamoto mpya kwingineko.

Akizungumza na tovuti rasmi ya Chelsea, Sterling alisema alifurahishwa na kurudi London.

"Ni wazi nimepata mafanikio mengi katika kazi yangu hadi sasa, lakini bado kuna mengi zaidi ya kufikia na ninasubiri kwa hamu kufanya hivyo nikiwa na jezi ya Chelsea, chini ya usimamizi wa Thomas Tuchel.

"London ni nyumbani kwangu na ambapo mambo yote yalianza hapa, na inashangaza kuwa sasa nina nafasi ya kucheza mbele ya marafiki na familia. Nasubiria kukutana na mashabiki hivi karibuni.

"Nataka kuchukua fursa hii kuwashukuru Todd, Behdad (kikundi cha umiliki), Thomas, na wote waliohusika katika mchakato wa kunifikisha hapa."

# Martinez akaribia kutua United

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United wamefikia makubaliano mapana na Ajax kwa ajili ya kumsajili Lisandro Martinez, kwa mujibu wa 90min.

Mashetani Wekundu hao awali walitoa ofa mbili kwa raia huyo wa Argentina, ambaye ana uwezo wa kucheza beki wa kati, pembeni na nafasi ya kiungo wa kati, na wamekuwa wakitaka kukamilisha dili hilo haraka iwezekanavyo huku Arsenal pia wakimwania.

Ajax wamekuwa imara katika mazungumzo na United, na wamejaribu kuongeza bei yake mara kadhaa, lakini nia ya kocha, Erik ten Hag kumleta Old Trafford imesababisha mazungumzo kuendelea.

Ajax ilikuwa na matumaini ya kuisogeza United karibu na euro milioni 60, lakini Martinez amefanya nia yake ya kuhama ijulikane zaidi kwa saa 48 zilizopita na kusababisha makubaliano kufikiwa.

Pia mazungumzo yanaendelea kwa fowadi wa Brazil, Antony pamoja na kiungo wa kati wa Barcelona, Frenkie de Jong, na wamejitahidi kufanya lolote katika mazungumzo kiasi kwamba mtendaji mkuu Richard Arnold na mkurugenzi wa soka, John Murtough kusafiri kwenda Hispania mapema wiki hii kufanya majaribio.



372,576/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 16/07/22 | 21:30 | Magdeburg vs Fortuna Dusseldorf | 3.03 | 3.37 | 2.28 |
| 02. 16/07/22 | 22:00 | AL Asyooti Sport vs Al Ahly Cairo | 3.16 | 3.16 | 2.29 |
| 03. 16/07/22 | 22:30 | Atletico Pr vs Internacional | 2.35 | 3.28 | 2.99 |
| 04. 16/07/22 | 22:30 | Sampaio MA vs Vasco da Gama | 2.87 | 3.01 | 2.57 |
| 05. 17/07/22 | 00:00 | Newell'S Old Boys vs Racing Club | 2.82 | 3.18 | 2.62 |
| 06. 17/07/22 | 00:30 | Guarani SP vs Bahia BA | 3.07 | 2.97 | 2.45 |
| 07. 17/07/22 | 01:00 | Avai vs Santos | 2.89 | 3.08 | 2.54 |
| 08. 17/07/22 | 03:00 | Ceara CE vs Corinthians | 2.40 | 2.99 | 3.19 |
| 09. 17/07/22 | 12:00 | Machida Zelvia vs V Varen Nagasaki | 2.47 | 3.10 | 3.00 |
| 10. 17/07/22 | 12:30 | Ryukyu vs Omiya Ardija | 3.14 | 3.24 | 2.31 |
| 11. 17/07/22 | 14:30 | Hansa vs Heidenheim | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 12. 17/07/22 | 16:00 | Wisla Plock vs Lechia Gdansk | 2.76 | 3.30 | 2.44 |
| 13. 17/07/226 | 17:30 | Servette Geneva vs St. Gallen | 2.34 | 3.74 | 2.69 |
| 14. 17/07/22 | 19:00 | Union Santa Fe vs Huracan | 2.76 | 3.06 | 2.76 |
| 15. 17/07/22 | 19:30 | EL Gouna FC vs Talaea El Gaish | 3.18 | 2.78 | 2.53 |
| 16. 17/07/22 | 22:00 | Nautico PE vs Chapecoense | 2.46 | 3.01 | 3.01 |
| 17. 17/07/22 | 22:00 | Arab Contractors vs Ceramica Cleopatra | 3.03 | 2.78 | 2.63 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 15/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1304 | Bangladesh Police Club vs Rahmatgonj Mfs | 1.95 | 3.93 | 3.00 |
| 13:00 | 1876 | Gwangju vs Anyang | 1.93 | 3.25 | 3.64 |
| 13:00 | 2300 | Madagascar vs South Africa | 5.29 | 3.33 | 1.64 |
| 13:05 | 3584 | Melbourne Victory vs Manchester Utd | 5.00 | 4.26 | 1.50 |
| 13:30 | 4677 | Gyeongnam vs Chungnam Asan | 2.36 | 3.20 | 2.75 |
| 14:00 | 1488 | Hai Phong vs CLB Viettel | 2.23 | 3.09 | 3.05 |
| 14:00 | 3347 | SQC Binh Dinh vs M. Nam Dinh | 1.85 | 3.05 | 4.33 |
| 14:00 | 3783 | Song Lam Nghe AN vs Hong Linh HA Tinh FC | 1.93 | 3.04 | 3.93 |
| 15:15 | 1328 | Sabah vs Johor Darul Takzim | 6.27 | 4.31 | 1.41 |
| 15:30 | 1099 | Torino vs Eintracht Frankfurt | 3.05 | 3.34 | 2.11 |
| 15:30 | 1970 | 1860 Munich vs Newcastle | 5.20 | 4.20 | 1.53 |
| 15:30 | 5174 | Union Berlin vs Ceske Budejovice | 1.28 | 5.30 | 7.85 |
| 15:35 | 5784 | Liverpool vs Crystal Palace | 1.35 | 4.82 | 6.68 |
| 16:00 | 4012 | Botswana vs Eswatini | 2.74 | 2.69 | 2.74 |
| 17:00 | 1250 | Namibia vs Mozambique | 2.50 | 2.74 | 2.99 |
| 17:00 | 4265 | CA Lanus vs CD Godoy Cruz | 1.54 | 3.94 | 5.12 |
| 18:00 | 1036 | Honka vs Lahti | 1.43 | 4.24 | 6.11 |
| 18:00 | 4613 | Shabab Al Ordun vs Al Sareeh | 1.84 | 3.34 | 3.89 |
| 18:00 | 4966 | Astana vs Shakhter Karagandy | 1.96 | 3.44 | 3.35 |
| 18:00 | 5838 | Paris St Germain vs US Quevilly Rouen | 1.21 | 5.82 | 9.70 |
| 18:00 | 5969 | BATE Borisov vs FK Arsenal Dzerzhinsk | 1.17 | 5.87 | 12.73 |
| 18:30 | 3338 | Hermanstadt vs CS Mioveni | 2.65 | 3.00 | 2.70 |
| 18:30 | 4032 | NK Posusje vs Velez Mostar | 2.20 | 2.94 | 3.28 |
| 19:00 | 1299 | OTP FC vs OLS Oulu | 2.59 | 3.57 | 2.30 |
| 19:00 | 1777 | Tammeka Tartu vs Levadia Tallinn | 10.83 | 5.51 | 1.21 |
| 19:00 | 4728 | Rakow Czestochowa vs Warta Poznan | 1.41 | 4.12 | 6.67 |
| 19:30 | 2799 | TSV Rain/Lech vs Schweinfurt | 4.32 | 3.93 | 1.63 |
| 19:30 | 5705 | SK Treibach vs Rapid Vienna | 34.40 | 15.73 | 1.01 |
| 20:00 | 2166 | Midtjylland vs Randers | 1.53 | 4.21 | 5.41 |
| 20:00 | 2826 | Illertissen vs Viktoria Aschaffenburg | 2.39 | 3.44 | 2.56 |
| 20:00 | 3855 | Zambia vs Senegal | 2.11 | 2.85 | 3.63 |
| 20:30 | 1288 | FC Schaffhausen vs FC Thun | 1.84 | 3.72 | 3.48 |
| 20:30 | 1619 | Yverdon-Sport FC vs FC Stade LS Ouchy | 2.69 | 3.28 | 2.36 |
| 21:00 | 1415 | Middlesbrough vs Sporting Braga | 3.67 | 3.67 | 1.80 |
| 21:00 | 1495 | Albion FC vs Deportivo Maldonado | 3.15 | 3.10 | 2.17 |
| 21:00 | 2479 | Spartak Subotica vs Radnik Surduluca | 2.15 | 3.20 | 3.10 |
| 21:00 | 4266 | Radnicki Nis vs Partizan | 9.60 | 4.90 | 1.26 |
| 21:00 | 5560 | Shrewsbury vs Burnley | 3.83 | 3.83 | 1.73 |
| 21:15 | 5577 | Besiktas vs Mainz | 2.64 | 3.86 | 2.16 |
| 21:30 | 1519 | Zaglebie Lubin vs Slask Wroclaw | 2.17 | 3.28 | 2.99 |
| 21:30 | 2706 | Chorley vs Stockport | 4.70 | 4.50 | 1.55 |
| 21:30 | 3433 | Universitatea Craiova vs Sepsi Osk | 2.25 | 3.10 | 3.20 |
| 21:30 | 3473 | Kaiserslautern vs Hannover | 2.41 | 3.25 | 2.80 |
| 21:30 | 3997 | Zemplin Michalovce vs Dukla Banska Bystrica | 1.80 | 3.54 | 3.83 |
| 21:30 | 4706 | Colchester vs Millwall | 4.11 | 3.86 | 1.67 |
| 21:45 | 3749 | Drogheda Utd vs Bohemians FC | 4.22 | 3.53 | 1.73 |
| 22:00 | 3360 | Austria W vs Norway W | 3.33 | 3.48 | 1.95 |
| 22:30 | 5896 | Santiago Morning vs Santiago Wanderers | 1.92 | 3.19 | 3.78 |
| 23:00 | 2827 | Benfica vs Nice | 2.32 | 3.43 | 2.65 |
| 23:30 | 2286 | Deportivo Municipal vs Club Cienciano | 2.90 | 3.34 | 2.20 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MSUVA, GAUCHO YAWAKUTA 'MAZITO' MOROCCO, WAONYA

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Waydad Casablanca ya Morocco imepewa siku 45 kukamilisha malipo ya Dola za Marekani 700,000 (sawa na Sh. bilioni 1.6) kwa aliyekuwa mchezaji wao, Simon Msuva baada ya nyota huyo kushinda kesi aliyofungua dhidi ya klabu hiyo.

Akizuñgumza jijini Dar es Salaam jana, Yasmin Razack, msimamizi wa mchezaji huyo alisema kiasi hicho kinatakiwa kulipwa mara moja na tangu hukumu hiyo itolewe, Wydad inaruhusiwa kukata rufani ndani ya siku 10.

Yasmin alisema Msuva amepitia wakati mgumu alipokuwa Morocco kwa kuwa hakuwa na usimamizi mzuri na kudai mchezaji anapofika nchini humo huwa ananyang'anywa hati ya kusafiria ili asipate msaada wowote ule.

Alisema Msuva alinyimwa haki zake mbalimbali huku akipewa makaratasi mengi ya kusaini ambayo yalikuwa yameandikwa lugha ya Kifaransa ambayo hakuifahamu lakini akilazimishwa kusaini haraka.

Aliwataka wachezaji wasikubali kusaini mkataba wowote bila kuwa na wanasheria binafsi ambaye atamtafuta kwa ajili ya kumsaidia hapo baadaye na kuongeza mateso aliyoyapitia Msuva yamekuwa fundisho.

Alisema mpaka Msuva amefanikiwa kushinda kesi yake amepata tabu hivyo Watanzania wanapaswa kufahamu Waarabu hawana utu.

Msuva alisema ameshukuru kushinda kesi hiyo na amewataka wachezaji wenzake kupata wasimamizi wazuri pindi wanapokuwa wanasaini mikataba na timu yoyote.

"Kwa mateso niliyoyapitia angekuwa mtu mwingine nisingeweza kuitumikia Timu ya Taifa lakini ninashukuru TFF pamoja na makocha wangu walikuwa wananishauri nitulize akili hatimaye nimefanikiwa na sitaki kulipwa pesa nusu nusu," alisema Msuva.

Aliongeza hali ilikuwa mbaya zaidi pale Rais wa klabu hiyo iliyomsajili kukata mawasiliano naye na kukataa kuonana naye hata pale alipomfuata nyumbani kwake.

"Kilichonikuta walinipa makaratasi mengi ya kusaini ambayo yalikuwa yameandikwa kwa lugha ya Kifaransa, nilisaini sikujua kile ambacho kitanikuta, sitaki kuwasikia Waarabu, nimeteseka mno," Msuva alisema.

Aliishukuru serikali pamoja na Watanzania kwa sapoti waliyompa kipindi chote alichokuwa kwenye matatizo hayo.

Wakati huo huo, Yasmin alisema mchezaji mwingine wa Tanzania, Mwanahamisi Omary 'Gaucho' naye ameamua kurejea nyumbani kufuatia klabu yake ya Shabab Atlas ya Morroco kutomtendea haki.

Mkurugenzi huyo wa Kampuni ya Tunzo, ambaye anamsimamia Gaucho alisema nyota huyo wa zamani wa Simba Queens ameisamehe klabu hiyo pesa zote anazozidai na hataki kurejea Morocco kuitumikia.



Msimamizi wa mchezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Simon Msuva, Yasmin Razack (kulia), akielezea namna nyota huyo alivyokuwa akiteseka nchini Morocco baada ya viongozi wa klabu aliyokuwa akiichezea ya Wydad Casablanca kumnyima stahiki zake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Beki Yanga aitaka Simba

**Na Saada Akida**

BEKI wa kati wa kimataifa wa Yanga Princess kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Daniela Ngoi ameweka wazi ameanza mazungumzo na Mabingwa wa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania, Simba Queens.

Akizungumza na gazeti hili jana akiwa kwao DRC, Daniela alisema amefikia uamuzi huo kutokana na kumaliza mkataba wake na Yanga Princess, lakini kutokuwa na wakati mzuri na klabu hiyo iliyomleta Tanzania msimu uliomalizika.

Daniela alisema kwa sasa yeye ni mchezaji huru baada ya mkataba wake wa mwaka mmoja kufikia tamati tangu Mei, mwaka huu.

"Ni kweli nilikuwa mchezaji wa Yanga Princess kwa msimu ulioisha, na mkataba wangu wa mwaka mmoja umemalizika, sasa narudi Tanzania kumalizana na uongozi wa Simba Queens ili kusaini mkataba mpya wa kutumikia klabu hiyo," Daniela alisema.

Aliongeza sababu nyingine iliyomfanya ajiunge na Simba Queens ni ofa nzuri waliyompatia na yeye yuko tayari kufanya nao kazi kwa sababu mpira wa miguu ndio kazi yake.

# Michezo

Ijumaa Julai 15, 2022
Nipashe



## Sterling rasmi mali ya Chelsea

UKURASA 22



Wachezaji wa Simba, Pape Sakho (kushoto) na Meddie Kagere wakiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana tayari kwa safari ya kuelekea Misri ili kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# HATIMAYE YANGA YAONYESHA KUBWA

●●●Ni baada ya Aziz Ki kutua nchini na kumalizana naye, sasa yajipanga...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HATIMAYE uongozi wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga umemalizana na mshambuliaji wake mpya wa kimataifa, Stephan Aziz Ki, ambaye alikuwa akisubiriwa kwa hamu na mashabiki wa timu hiyo katika msimu mpya, imefahamika.

Usajili wa Aziz Ki, raia wa Burkina Faso kutoka Asec Mimosas ya Ivory Coast umekuwa gumzo na kuzua sintofahamu mbalimbali kutokana na kutajwa mchakato wake umeingia dosari.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Sakaam jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema nyota huyo ni mali ya klabu yao na amewasili nchini tangu juzi kwa ajili ya kutambulishwa rasmi.

Bumbuli alisema Yanga ilimalizana na Aziz Ki muda mrefu na sababu iliyochelewesha nyota huyo kutambulishwa mapema ilikuwa nje ya uwezo wao.

"Aziz Ki yuko hapa nchini, amesaini mkataba wa kuichezea Yanga ila kilichokwamisha ni utambulisho kwa sababu walikuwa hawajamalizana na klabu yake, lakini alienda likizo, jambo ambalo hatukuwa na haraka ya kumtambulisha na kumsubiri afike nchini," alisema Bumbuli.

Aliongeza amewasili nchini kwa ajili ya kuingia kambini kuanza maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki.

Alisema pia mshambuliaji huyo atavaa jezi namba 10 iliyokuwa ikivaliwa na Yacouba Sogne, ambaye amemaliza mkataba na klabu hiyo.

"Mnakumbuka Rais wetu Injinia Hersi Said alipokwenda alikutana naye, na nadhani mmesahau tulithibitisha amesaini, lakini utambulisho wake ulikuwa unasubiria masuala ya msingi.

Kwanza tulikuwa tunasubiri mkataba wake umalizike tarehe 13, mwezi huu, halafu asingeweza kuja wakati wenzake wapo mapumziko, ilikuwa ni lazima asubiri wachezaji waanze kukusanyika na yeye ndiyo aje, halafu sisi utambulisho wetu ni lazima kwanza mchezaji afike kwanza ndiyo tumtangaze," alisema Bumbuli.

Alisema kwa sababu kila kitu kimekamilika, na wanaweza kumtangaza wakati wowote huku akisema ndiye atakuwa mchezaji wa mwisho kwa msimu huu kusajiliwa, ikiwa imesajili wachezaji watano tu, wote wakiwa wa kigeni.

"Wanachama na mashabiki wa Yanga wasiwe na wasiwasi tutawaeleza huyu mchezaji wa mwisho tuliyemsajili tumtambulishe ni nani, anatokea wapi na baada ya kumtambulisha tutaanza sasa kuwaeleza mchakato mzima ulivyofanyika hadi kumnasa, mchezaji kama huyu ni lazima mgombee klabu nyingi, siyo unamkosa unasema hutukuwa na haja naye," Bumbuli alibainisha.

Mpaka sasa Yanga imeshamtambulisha Joyce Lomaliza kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Mrundi Gael Bigirimana, Lazarous Kambole wa Zambia na Bernard Morrison akitokea kwa watani zao, Simba.

Wakati huo huo, Yanga jana ilitangaza kuachana na nyota wake, Deus Kaseke ambaye msimu uliomalizika hakupata nafasi nzuri ya kucheza.

Yanga imemtakia kila la kheri mchezaji huyo ambaye huenda akajiunga na Singida Big Stars (zamani DTB FC) ya mkoani Singida ambayo itashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

## Simba safarini Misri na M-Bet

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI ikiwatangaza M-Bet ndio wadhamini wakuu wapya wa timu yao, kikosi cha Simba chenye wachezaji 19 kiliondoka nchini jana jioni na kuelekea Misri kwa ajili ya kuweka kambi ya muda wa wiki tatu kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola alisema jana muda mfupi kabla ya kuanza safari kuwa wakiwa huko wanatarajia kucheza michezo mbalimbali ya kirafiki kujiweka tayari kupambana katika msimu mpya ambao pia utakuwa mgumu na wenye ushindani.

"Tunaondoka na wachezaji 19, tukiwa huko tunatarajia kupata michezo ya kirafiki, hiyo iko katika programu iliyowekwa na kocha wetu mkuu," alisema Matola.

Kiungo na nahodha huyo wa zamani wa Simba alisema wanaondoka bila ya nyota wake walioitwa katika Timu ya Taifa (Taifa Stars), lakini baada ya kumaliza majukumu yao wataungana na kikosi hicho huko Misri kuendelea na maandalizi.

"Wachezaji wengine wamebaki kwenye timu ya taifa, wakimaliza majukumu yao watakuja Misri kuungana na sisi kwa ajili ya kujiwinda na msimu ujao, tunajua utakuwa na changamoto na ushindani zaidi, tunahitaji kujiimarisha ili kufanya vizuri," Matola alisema.

Alieleza wameshindwa kuondoka na mchezaji wao, Yusuph Muhilu kwa sababu bado alikuwa anaendelea na mazungumzo na uongozi wa klabu hiyo na watakapofikia muafaka wataweka wazi.

"Usajili wetu kwa asilimia 99 umekamilika, tunawaomba mashabiki wetu wawe na subira, kila atakayesajiliwa atawekwa hadharani," Matola alisema.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally alisema watakaa Misri kwa muda wa wiki tatu na baada ya hapo watarejea nchini kwa ajili ya Tamasha la Simba Day na kuanza msimu mpya.

Mshambuliaji Mnyarwanda, Meddie Kagere alisema wanakwenda kujiandaa na msimu mpya ambao anaamini utakuwa mgumu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >